30 OKTOBA, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Nne – Tarehe 30 Oktoba, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 35 la tarehe 28 Agosti, 2026;
2. Toleo Na. 36 la tarehe 04 Septemba, 2026;
3. Toleo Na. 37 la tarehe 11 Septemba, 2026;
4. Toleo Na. 38 la tarehe 18 Septemba, 2026;
5. Toleo Na. 39 la tarehe 25 Septemba, 2026;
6. Toleo Na. 40 la tarehe 02 Oktoba, 2026;

7. Toleo Na. 41 la tarehe 09 Oktoba, 2026;
8. Toleo Na. 42 la tarehe 16 Oktoba, 2026; na
9. Toleo Na. 43 la tarehe 23 Oktoba, 2026.

SPIKA: Ahsante.

MAELEZO YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Maelezo ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuhusu Ununuzi na Matumizi ya Magari katika Utumishi wa Umma.

Waheshimiwa Wabunge, Utangulizi; kabla ya kutoa maelekezo yangu ninaomba nirejee maelezo yaliyopo kwenye ukurasa wa 108 hadi 110 wa Taarifa ya Mapendekezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Serikali maarufu kama "*Chenge One Report.*" Nanukuu…

(a) Ununuzi wa magari makubwa na ya anasa usiozingatia gharama za uendeshaji wake na hali yetu ya kiuchumi na gharama zingine zisizo za lazima Serikalini zingeweza kupunguzwa kufikia robo au pungufu zaidi kama magari yenye injini ndogo yangetumika na matumizi yasiyo ya lazima kudhibitiwa ili gharama hizo zilingane na hali ya uchumi wa Taifa na kauli za Viongozi wa Serikali. Kuhusiana na hali kama hii, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo K. Pinda, akiahirisha Mkutano wa Tisa wa Bunge, tarehe 9 Novemba, 2012 alisema:-

"…Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kuwa kwa mara kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu nimekuwa nikieleza nia ya Serikali ya kubana matumizi yasiyo ya lazima wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

…nchi yetu ni masikini, hivyo, hatuna budi kutumia kiasi kidogo cha fedha zilizopo kuondokana na umasikini huo na kuwa nchi yenye angalau uchumi wa kati. Kwa mfano, nimekuwa nikizungumzia kupunguza ununuzi wa magari ya kifahari kama vile *Toyota Landcruiser VX*. Zipo *Toyota Landcruiser VX 8 - High*

Specifications na *Toyota Landcruiser VX 8 - Standard*. Bei ya *VX 8 - high specifications* ni zaidi ya shilingi milioni 300 kwa gari moja. Kiasi hicho pekee kinatosha kujenga zahanati moja na nyumba mbili za watumishi. *(Makofi)*

Aidha, kiasi hicho kinatosha kujenga nyumba sita za watumishi wa vituo vya afya au kujenga madarasa 17 ya shule za msingi. Kiasi hicho hicho kinatosha kununua madawati 2,500 ya kukaliwa na wanafunzi watatu watatu, au kununua vifaa vya Maabara katika Shule za Sekondari na hali kadhalika. Hivyo, mtaona kuwa tukiacha kununua gari moja la *VX-8* tunaweza kusaidia jamii ya Watanzania kwa kiasi kikubwa zaidi…" Mwisho wa kunukuu.

(b) Aidha, mtazamo huu wa Kamati unaungwa mkono na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Taarifa yake kwa Kamati inayoeleza kuwa "Serikali iondokane na matumizi ya magari ya anasa na iweke utaratibu wa kutumia magari yenye injini zenye *capacity* ndogo kama ilivyo kwa Nchi za Rwanda, Ethiopia na Kenya na zingine". Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 14 Juni, 2022 aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu ambaye hivi sasa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akiwasilisha Hotuba ya Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 alisema masuala yafuatayo kuhusu kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ikiwa ni pamoja na matumizi ya magari na mafuta, kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. Nanukuu…

"Mheshimiwa Spika, mkakati wa kubana matumizi; kwa upande wa Sera za Matumizi katika mwaka 2022/2023, sera zitakuwa za kubana na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali inatarajia kudhibiti ununuzi na matumizi ya magari kwa kuzingatia Waraka wa Rais Na.1 wa mwaka 1998 kuhusu hatua za kubana matumizi ya Serikali na Waraka Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.2 wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina za stahili za magari

kwa viongozi katika utumishi wa umma ili kubana matumizi. Hapa mlipiga makofi mbona leo hampigi? Maana imeandikwa kwenye *Hansard* hapa makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yenye gharama kubwa sana kwa Serikali ni ununuzi wa magari, ununuzi wa mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri na matengenezo. Tunapanga kuchukua hatua za muda mfupi na za muda mrefu. Lazima matumizi ya Serikali na matumizi ya watumishi wa umma yote yaakisi ugumu wa maisha wanayoyapata wananchi wetu, kufuatia athari za majanga hususan UVIKO -19 ili fedha zinazopatikana ziweze kufanya mambo muhimu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua za muda mfupi zitakazochukuliwa ni pamoja na kupunguza safari za ndani na nje, kukata fedha za ununuzi usio wa lazima, kupunguza ukubwa wa uwakilishi kwenye mikutano ya ndani na nje, tutapimiana mafuta ya magari ya Serikali kila mwezi kufuatana na shughuli za lazima. Utaratibu huu unatumika hata kwa Wabunge na hawajawahi kuacha kufanya ziara, ndiyo utaratibu pia unaotumika kwa Benki Kuu na baadhi ya Taasisi za Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemwelekeza Mlipaji Mkuu wa Serikali afanye uchambuzi wa wastani wa mahitaji ya mafuta kufuatana na aina ya majukumu, ulazima wa majukumu pamoja na ngazi katika utumishi. *(Makofi)*

Kwa upande wa hatua za muda wa kati na za muda mrefu, ninapendekeza Serikali kubadili kabisa utaratibu uliopo ili kuwakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari la Serikali wawe na magari yao wenyewe wayalipie, wafanye matengenezo wao wenyewe, wanunue vipuri wao wenyewe na masuala ya mafuta yaangaliwe kwa utaratibu utakaoonekana unafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia, ninapendekeza Serikali kubadili kabisa utaratibu uliopo ili kuwakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari la Serikali. Wakopeshwe na walipe,

wakishalipia magari yale yanakuwa ya kwao, wafanye matengenezo wao wenyewe, wanunue vipuri wao wenyewe na masuala ya mafuta yaangaliwe kwa utaratibu utakaoonekana unafaa. Hayo maneno ya Waziri Mkuu siyo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ina magari zaidi ya 15,742, pikipiki zaidi ya 14,047 na mitambo 373 na inatumia zaidi ya shilingi 558,000,000,000 kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi, ununuzi wa mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri pamoja na matengenezo. Ukiondoa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na Mahakama, upande wa Serikali unabaki na viongozi wakuu wachache wa kila Wizara, Mashirika, Wakala, Mikoa, Wilaya pamoja na miradi ambayo inahitaji usimamizi na wasimamizi wanatakiwa kuwa katika maeneo ya mradi yaani kuwa kule *(site)* kwa muda mwingi, ambapo kwenye makundi haya hawatazidi watano kwa Taasisi na wengine wote wenye stahili za kuwa na magari wakopeshwe, watumie magari yao, watasimamia vizuri matumizi ya magari hayo, watasimamia vizuri matengenezo, watasimamia vizuri mafuta na watasimamia vizuri vipuri.

Tutaondoa utaratibu uliozoeleka, dereva na gari anapitishwa chini, bosi anapanda ndege labda kutoka Mwanza au Mbeya anasema tukutane Dar es Salaam na kurudi hivyo hivyo. Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 23 Juni, 2026, Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omari, Waziri wa Fedha, wakati akihitimisha hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2026/2027 aliwasilisha masuala mbalimbali yenye nia ya kupunguza matumizi ya Serikali ikiwemo ununuzi wa magari. Nanukuu…

"Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ambalo limejitokeza sana katika michango hii, ilikuwa ni ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na ushauri wa Kiti chako, kwenye haja na umuhimu wa haraka wa Serikali kupunguza matumizi yake, hasa matumizi yasiyo ya lazima. Limezungumzwa suala la ununuzi na matumizi ya magari ya gharama nafuu, lakini pamoja na matumizi yenyewe ya magari;

limezungumzwa suala la safari za ndani na nje ya nchi na ushiriki wa mikutano ambayo mingine isiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa vilevile uwezekano wa kubana matumizi kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.5 ili fedha hizo zielekezwe katika ulipaji wa madeni ya wakandarasi na huduma nyingine za afya za kijamii." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, aidha, tarehe 4 Septemba, 2026 Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akiwasilisha Hoja ya Kuahirisha Bunge kwenye Mkutano wa Nne, Kikao cha Nane alieleza masuala mbalimbali kuhusu kubana matumizi ikiwa ni pamoja na kupunguza misafara. Kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge alieleza masuala yafuatayo na nanukuu: -

"Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo, Waziri wa Fedha alitoa rai kubana matumizi na kuelekeza fedha kwenye vipaumbele. Kwa kuzingatia hilo, ninaelekeza hatua zichukuliwe katika maeneo yenye fursa za kupunguza matumizi bila kuathiri ufanisi wa shughuli za Serikali. Maeneo haya ni pamoja na matumizi ya uendeshaji wa magari ya Serikali, matumizi ya shajara, gharama za safari za ndani na nje, gharama za michakato ya bajeti kwa kupunguza idadi ya watumishi wanaoshiriki, gharama za mikutano, warsha, makongamano pamoja na safari nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, bado tuna fursa ya kupunguza haya. Ninayo mifano, nitatoa mfano mmoja. Ningali Mbunge, ninakumbuka nimewahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*, katika Bajeti ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wote na *CMT* zote, Kamati za Fedha wote wanakuja nchi nzima. *CMT* ile ina watu kama 14, ukiweka na Wakurugenzi, ukiweka na Mkoa, maana yake ni kama mkoa mmoja wanakuja watu 100 mpaka 180. Kwa nchi nzima ni kama watu 5,500 mpaka 6,000.

Mheshimiwa Spika, wanaoingia pale kwenye chumba kile cha Kamati kuonana na Kamati ya Bunge, wanaoongea,

wakiongea wengi ni watatu mpaka wanne. Wengine wote wanasubiria nje. Haya ni mambo ya mazoea ambayo tunaweza tukayaepuka na fedha hizo tukazipeleka kwenye ujenzi wa madarasa ambayo yatahitajika sana tunapoanza utekelezaji mpya kwa mageuzi ya elimu. Hivyo ni vitu ambavyo tunaweza tukavipunguza bila hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshuhudia hata kwenye ziara, ni vitu vya mazoea, vimezoeleka. Unaenda kwenye Mkoa A ambapo utaenda Wilaya zote, lakini kwenye Wilaya zote Watendaji wa Mkoa mzima, hata wilaya ambayo hatuendi wote nao wanakuja. Matokeo yake mnaenda kukagua darasa lililojengwa kwa shilingi 24,00,000, lakini mnaenda na magari 150. Ndiyo hapo sasa gari la Mbunge linakuwa la 151. Tunakagua actually magari 150, mradi wa shilingi 24,000,000. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, awaelekeze Wakuu wa Mikoa pamoja na idara mbalimbali, haya ni mambo tunaweza kuyaepuka. Wanaenda kwenye bajeti, wazimalize kule kule mikoani. Afisa Masuuli ambaye ni Katibu Tawala na Mkuu wa Mkoa na Afisa Bajeti waende kukutana na Kamati. Mbona tukienda kukutana na *IMF, World Bank* unakuta wao wako wawili tu, sisi tuko 50. Wao wako wawili tu, tena kukutana na Balozi, unakutana na Balozi na Msaidizi wake. Ninyi mko 33, mnakaa upande wenu, mnazunguka mpaka na upande wao. Haya ni mambo ya mazoea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Katibu Tawala wa Mkoa aisome bajeti ya mkoa wake, Mkuu wa Mkoa atafungua, atakaribishwa, atakaribisha wataalamu waliotoka mkoani kwake. Katibu Tawala na Afisa Bajeti wazisome bajeti wazielewe. Huu utaratibu wa kuleta watendaji wote nchi nzima, Halmashauri zote 184, wakija na magari matatu matatu ni magari zaidi ya 500, kuingia na yanatumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, mkutano mmoja wa kuangalia bajeti, wanaoongea watu watatu tu zinatumika zaidi ya shilingi 20,000,000,000. Tunahitaji shilingi 20,000,000,000 tu kujenga

madarasa yote haya tunayohitajika ili tuweze kukamilisha mageuzi katika elimu. Hii inakosa *flow* kwa sababu ni *Hansard* na *Hansard* wanapokea saa nyingine nao wana… *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa anatosha na wilaya husika kupokea. Wilaya zote zinaenda kumpokea! Wote! taasisi zote, ofisi zinafungwa kwanza. Yakipita magari, ni kama wale nyumbu wanahama kutoka Tanzania wanaelekea nchi jirani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haya ni ya mazoea tu, tunaweza tukayabadilisha. Hasa hasa, siyo kwamba sipendi watu wasafiri, tuna jambo kubwa ndugu Watanzania. Kuanzia 2028 tunatarajia watoto wanaokwenda kuanza *form one* wawe mara tatu ya wale wanaokwenda kuanza *form* one kila mwaka. Walikuwa wakianza 900,000, sasa wanaenda kuanza zaidi ya 3,000,000. Mwisho wa kunukuu…

Waheshimiwa Wabunge, Ibara 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatamka kwamba Bunge litakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. Aidha, Ibara ya 63(3)(a), (b) na (c) inaweka masharti ya namna ambavyo Bunge linaweza kutekeleza madaraka yake.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo, kwa kuwa imepita takribani miaka 13 tangu kutolewa kwa "Ripoti ya Chenge One" na kwa kuwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Pinda, ya Waziri wa Fedha Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na tena Waziri Mkuu mwenyewe hayajafanyiwa kazi na baadhi ya taasisi na mamlaka zote za Serikali. Hivi juzi Mheshimiwa Makamu wa Rais naye kasema tujibane na tujinyime, sasa Bunge hatujibani tutabidi tujinyime.

Ninatoa maelekezo yafuatayo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kufanya kikao cha pamoja na Wizara ya Fedha,

Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Wizara ya Ujenzi pamoja na Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali kwa muda wa siku kadhaa ambazo tutaziweka ili kuchambua na kutoa ushauri kwenye masuala yafuatayo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2023 hadi mwaka 2026:-

(i) Kufanya uchambuzi wa gharama za ununuzi, matumizi ya mafuta na ukarabati wa magari ya Serikali kwa kipindi cha miaka kumi na tatu (13) kuanzia 2013 - 2026;

(ii) Kuangalia namna ambavyo Serikali inaweza kupunguza matumizi ya mafuta kwa kuangalia ukubwa wa injini, aina ya gari pamoja na matumizi ya nishati nyingine jadidifu kama vile umeme na gesi asilia. Hii ni pamoja na kuweka mikakati ya kuepuka ununuzi wa magari yenye injini kubwa, kuachana na yaliyopo na kujikita kwenye ununuzi wa magari yanayotumia mfumo wa gesi na mafuta/umeme na mafuta ambayo yanaitwa *hybrid*.

(iii) Kupitia miongozo yote ya Utumishi wa Umma kuhusu ununuzi wa magari ya Serikali pamoja na mfumo wa uuzaji kwa magari chakavu. Mfano; Waraka Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2021 kuhusu Utaratibu wa Matumizi, Aina na Stahili za Magari kwa Viongozi katika Utumishi wa Umma. Hata hivyo, imebainika kwamba waraka huu unapuuzwa na baadhi ya Mashirika, Taasisi na Wizara mbalimbali za Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, hii ni taarifa Spika na hali sasa hivi ni mbaya duniani kote kuhusu mafuta na gharama za maisha ambazo Tanzania tunapitia. Lazima tujibane tupunguze gharama. Maelekezo mengine, wote waliokiuka Waraka wa Utumishi wa Umma 2021 wa kununua magari bila kufuata taratibu za kisheria za Kiserikali, kutokuwa na stahiki ya kuwa na aina fulani ya gari, lakini ukajinunulia gari unalolitaka wewe mwenyewe. Wote waitwe na hii Kamati, wahojiwe na hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao. *(Makofi)*

Tunawapa muda mpaka Bunge lijalo la Januari, Kamati iwe imeshamaliza na Serikali, mtuletee taarifa rasmi ndani ya Bunge ili tujue hatua ambazo zimechukuliwa kuokoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais ametoa mfano, kupunguza misafara yake. Wataalamu wake sasa wanapanda basi; wanaingia wote kwa pamoja kwenye basi. Mnaona ninyi mitaani kama kuna misafara mingine mikubwa ya kitaifa ambayo wageni wanakuja, usalama unaongezeka na utakuta magari yanaongezeka, lakini ziara zake mwenyewe za ndani zote amezidhibiti. Kama Mheshimiwa Rais kazidhibiti sisi tunangoja nini? *(Makofi)*

Hata mimi nishampa maelekezo Katibu wa Bunge, kubadilisha magari ya ofisi yangu. Tunangoja tu magari ya *hybrid* ya bei chini ya shilingi 100,000,000 ndiyo tutakayoyatumia. Kama Mheshimiwa Spika anatumia magari ya bei ya chini, sijui kwa nini Mheshimiwa Waziri unataka kutumia gari ya shilingi 400,000,000. Sijui kwa nini? *(Makofi)*

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Chacha Mwita.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti

Na. 44

Kuimarisha Sekta ya Afya – Geita Mjini

MHE. CHACHA M. WAMBURA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha sekta ya afya kwa kuongeza vituo vya afya, madaktari, wauguzi na vifaa tiba - Geita Mjini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za afya hususan ngazi ya afya ya msingi kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya afya, kuajiri watumishi wa kada za afya, pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026, Serikali imeajiri jumla ya watumishi wa kada ya afya 11,198 ambapo watumishi wa kada ya uuguzi walioajiriwa walikuwa 6,450 na Halmashauri ya Mji wa Geita ilipangiwa jumla ya watumishi wa afya 109.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 56.25 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa hospitali na shilingi bilioni 23.37 kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo vya afya 111 kote nchini. Aidha, Halmashauri ya Mji wa Geita imetengewa jumla ya shilingi 170,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga jumla ya shilingi 405,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba, ambapo Mkoa wa Geita umetengewa jumla ya shilingi bilioni 7.28 na Manispaa ya Geita imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.09.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura, swali la nyongeza.

MHE. CHACHA M. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Ninaishukuru sana Serikali, lakini ninaipongeza kwa jinsi ambavyo kwa kweli inachukua hatua mbalimbali kuhakikisha hii sekta ya afya inaenda vizuri. Hata hivyo ninaipongeza pia na ninaishukuru kwa kupandisha vituo vipya vinne kuwa vituo vya afya, lakini kwenye hivi vituo tuna changamoto kama mbili. Ninaomba kuuliza haya maswali mawili nipate majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa Jimbo zima la Geita Mjini tunazo *ambulance* katika vituo viwili tu. Vituo vingine vyote vilivyobaki havina *ambulance*. Ukiangalia jinsi ambavyo jiografia imekaa, kiukweli ni kwamba ni vigumu sana *ambulance* kutoka kituo kimoja kwenda kufuata mgonjwa kituo kingine na kumpeleka pale inapokuwa wanatakiwa kupata *referral*. Sasa ninaomba nijue majibu ya Serikali. Ni mkakati gani upo kuhakikisha kwamba tunapata *ambulance* kwenye vile vituo vingine vya afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; katika hivi vituo tulivyopandisha hadhi na kuwa vituo vya afya ambapo kwa kweli ninaishukuru sana Serikali kwa kupandisha, tuna changamoto ya watu wa *radiology* (watu wa mionzi). Pamoja na kwamba miundombinu imekamilika, kila kitu kiko vizuri, lakini hatuna hao wataalamu mpaka sasa hivi. Je, Serikali haioni kwamba tunatakiwa kulichukua jambo hili kwa udharura wake tuweze kuajiri hawa wataalamu wa mionzi ili basi watu wa Geita Mjini waweze kupata hii huduma muhimu katika vituo hivi vya afya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura, Mbunge wa Geita Mjini kwa namna ambavyo anafuatilia maendeleo na yeye mwenyewe amekuwa akishiriki na tumekuwa tukimwona katika *clips* mbalimbali akisaidiana na wananchi kusukuma mbele maendeleo ya Jimbo la Geita Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza na swali la kwanza, sote ni mashuhuda kwamba Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi hiki kifupi tumesambaza jumla ya magari 370 ya wagonjwa, lakini kwa magari yote kwa ujumla ambayo tunayo katika halmashauri zetu, ni magari 1,765. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura kwamba katika magari haya, halmashauri zetu zina idadi ya wastani wa magari mawili mpaka matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa yale mengine ambayo yanakuwa yameharibika lakini Wakurugenzi wanakuwa hawaja-*take action* ya kufanyia matengenezo, ninatoa maelekezo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wote nchini wahakikishe kwamba magari ambayo yameharibika yanatengenezwa na yaende yakafanye kazi ya kutoa huduma kwa wagonjwa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Wambura kwamba, tutaendelea kutenga bajeti kulingana na tunavyopokea magari kutoka Wizara ya Afya, lakini pia Serikali inashirikiana na *Global Fund* na kushirikiana pia na *Team Chip*, kadiri tunavyoyapokea magari haya tutaendelea kuyaelekeza na kumpa kipaumbele Mheshimiwa Mbunge angalau apate gari katika zile kata zake za pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, linahusiana na wataalamu wa afya. Serikali imeendelea kuajiri wataalamu wa afya hasa wale wataalamu wa mionzi, lakini bado hawatoshelezi katika maeneo mengi nchini. Tumepeleka maelekezo kwa Wakurugenzi lakini pia *RMOs* na *DMOs*, kwanza kuwashawishi wale wataalamu wa afya walio katika vituo vyao vya afya na kuwalipia mafunzo maalumu ya muda mfupi ili waende wakakidhi mahitaji ya kuhakikisha wagonjwa wetu wanapata huduma za kiradiolojia na uchunguzi kama huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahakikisha tunaendelea kuongeza wataalamu katika vituo vyetu ili wakatoe huduma zinazoleta tija katika vituo vyetu vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza ninaishukuru Serikali kwa kututengea pesa shilingi 700,000,000 pale Manyamanyama. Pia, ninashukuru tena kuna pesa shilingi 800,000,000 zilihimizwa zikaja kwenye hospitali yetu ya halmashauri ya mji. Ninaomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Bunda Mjini lina kata sita ambazo ziko pembezoni na zimekidhi vigezo vya kuwa na kituo cha afya: Kata za Guta, Kabasa, Mcharo na Sazira ni maeneo ambayo yana watu wengi ambao wanakwenda umbali mrefu kwenda kufuata huduma za afya Manyamanyama pamoja na Kituo cha Afya cha Bunda Mjini. Je, ni lini sasa watatujengea vituo vya afya katika hizo kata ili wananchi wa Bunda Mjini wapate huduma za afya kwenye maeneo yao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Ester kwa kushukuru na muungwana lazima ushukuru kwa fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.2 ambazo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imepeleka kwenye vituo vya afya, lakini na kwenye ile hospitali yetu ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama tulivyoanza kwenye vituo ambavyo alivianisha hapo awali na hivi ambavyo amevitaja, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutavichukua kuhakikisha kwamba katika bajeti ijayo tunaviwekea kipaumbele kwa kuvitengea bajeti kuhakikisha kwamba baadhi ya vituo ambavyo amevitaja viende vikatoe

huduma hasa vile ambavyo vinaonekana ni vituo vya afya vya kimkakati ambavyo vinahudumia zaidi ya kata moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea fedha Wilaya ya Mbarali kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya ambapo ilituletea kiasi cha shilingi bilioni 4.5. Vilevile, akaleta fedha kiasi cha shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kunatokea changamoto kwenye vituo vya afya. Kuna Kituo cha Afya cha Mawindi kilianza kujengwa tangu mwaka 2012 mpaka sasa hivi hakijakamilika. Pia, Kituo cha Mapogoro bado hakijakamilika. Sasa je, ni lini vituo hivyo vitakamilika ili wananchi wa Wilaya ya Mbarali waweze kupona?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya na anafuatilia kweli masuala haya ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameanza kwa ushuhuda ambapo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejizatiti kuhakikisha kwamba huduma ya afya inakuwa bora nchini. Ndiyo maana mpaka leo tunapozungumza hapa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiye *champion* wa masuala ya afya Barani Afrika kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tulifanya tathmini ya jumla ya vituo vya afya 111 na tayari tumeshaomba fedha zaidi ya shilingi 23,000,000,000 ambazo tutazielekeza katika vituo hivi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Fyandomo nikuondoe shaka katika vituo hivyo, baada ya kukamilisha zile hospitali za wilaya, twende sasa kwenye vituo hivi na tutavitengea fedha ili tukamilishe miundombinu ambayo Mheshimiwa Mbunge amehitaji ili ikatoe huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hili swali lina maswali ya nyongeza karibu 15. Kwa hiyo, kwa watakaopata nafasi waulize swali kwa ufupi.

Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES A. HOKORORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Mkoa wa Mtwara, kwanza tunaipongeza Serikali kwa kuwa imewezesha kujenga Hospitali ya Kanda ya Mitengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu dogo ni kwamba, katika Mkoa wa Mtwara kuna upungufu mkubwa wa madaktari na wauguzi katika halmashauri zote tisa. Kama kuna halmashauri ina wahudumu wa afya, sana sana ni kwa 38.8% kwa mkoa mzima. Je, Serikali pamoja na kwamba imejenga vituo vya afya, hospitali ya kanda, hospitali za mkoa na kuimarisha hospitali za wilaya, huduma zinazotarajiwa kupatikana kutokana na watabibu na wauguzi zinakuwa ni kwa kiasi kidogo. Je, tuna mpango gani sasa kuimarisha upatikanaji wa watumishi hao hasa kwenye maeneo ya pembezoni katika Mkoa wa Mtwara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Hokororo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza kwa kuwasemea wananchi wa Mtwara ili waweze kupata huduma ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anataka iende kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiajiri watumishi wa afya na kuwapanga katika halmashauri zote na mikoa yote nchini kwa msawazo na hasa katika mikoa hii ya pembezoni, baadhi ya watumishi wamekuwa hawaendi au wakienda, wakifika wanaripoti na kuanza kuomba uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa watumishi ambao wanapangwa katika halmashauri zetu hizi za pembezoni, kuhakikisha wanakwenda kufanya kazi ya kuwatumikia Watanzania. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora alitoa maelekezo mahususi kwamba hakutakuwa na uhamisho hadi ukidhi vigezo vya kukaa katika kituo chako cha kazi. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Hokororo na wananchi wa Mtwara, tutaendelea kuwapanga watumishi katika maeneo haya, lakini pia Wakurugenzi waendelee kutoa ajira za mkataba kwa watumishi wale ambao wanajitolea katika maeneo haya ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Innocent Bashungwa, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, ninaishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya ya kuboresha sekta ya afya katika Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua unafahamu jitihada kubwa za wananchi wa Kata ya Ihembe wakishirikiana na mimi Mbunge wao, tumejenga kituo cha afya mpaka ngazi ya *lintel* na nimekuwa nikiiomba Serikali itusaidie kukamilisha kituo hicho cha afya. Je, ni lini Serikali itatusaidia kukikamilisha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninampongeza kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa kwa kuleta swali hili la nyongeza na alishawahi kuuliza kwenye lile Bunge lililopita kwenye vituo vingine vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Bashungwa pamoja na wananchi wa Jimbo la Karagwe kwamba tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tulitenga kiasi cha shilingi 500,000,000. Ninamwelekeza tu Mkurugenzi wa halmashauri ampe ushirikiano wa dhati katika fedha hizi ambazo tumezitenga ambazo zinakwenda katika mwaka huu wa fedha 2026/2027 ili zikalete tija na wazielekeze katika maeneo haya ya ukamilishaji ili vituo hivi vianze kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tunaishukuru Serikali kwa kutujengea Kituo cha Afya katika Kata ya Hirbadaw toka mwaka 2019. Tunaishukuru Serikali kwa kutujengea jengo la kuhifadhia chumba cha watu wanaotangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka 2019 jengo lilipokamilika, hakukuwahi kuletwa vifaa kwa ajili ya kuhifadhia miili. Sasa, ni lini Serikali itakamilisha kazi kubwa ambayo imeshafanya ya kujenga jengo na wananchi waweze kupata huduma? Kwa sababu kwa sasa, wananchi wanakwenda kuhifadhi miili katika Mkoa wa Singida takriban kilometa 56. Je, lini sasa Serikali itatuletea vifaa hivi ili wananchi hawa waweze kupunguza makali ya umbali wa barabara na kuweza kuhifadhi katika eneo lao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, kama ambavyo ameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, tumekwishafanya mawasiliano ya ndani na *MSD* ili kuweza kupeleka jokofu. Mheshimiwa Mbunge anaongelea jokofu la kutunza miili katika *mortuary* ambayo tayari miundombinu ya jengo tumeshajenga. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tunaendelee kuwasiliana na Wizara yetu ya Afya kuhakikisha kwamba jokofu lile linafika kwa wakati ili kupunguza adha ya wananchi kupeleka miili katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo letu la Kilolo, kuna Kata ya Ibumu, Image, Irole, Bomalang'Ombe na Kimala. Hizi kata ziko mbali sana na hospitali ya wilaya na wananchi wanateseka sana kufuata huduma. Je, ni lini sasa vituo vya afya vitajengwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, kama ambavyo ameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo ya jimbo lake na kuwatakia mema wananchi wake hasa katika eneo la afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri aweze kutuandikia andiko maalumu la vituo hivi ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviainisha ili Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tuanze kutenga bajeti na kuhakikisha kwamba tunavijenga ili vikalete huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 45

Uhitaji wa Wodi ya Watoto Kituo cha Afya cha Mjimwema

MHE. MARIAM M. NYOKA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga wodi ya watoto katika Kituo cha Afya cha Mjimwema kilichopo Manispaa ya Songea?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Ruvuma kuwa Kituo cha Afya Mjimwema kimejengwa mwaka 2001. Kituo hiki kina upungufu wa miundombinu ya jengo la maabara, jengo la mionzi, wodi za kulaza wagonjwa na wodi ya wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Mjimwema ni miongoni mwa vituo vya afya Kongwe 358 vilivyofanyiwa tathmini ambavyo vinahitaji kufanyiwa ukarabati pamoja na kuongezewa miundombinu ya msingi ili viweze kutoa huduma stahiki ngazi ya kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya Kongwe kote nchini ambapo jumla ya shilingi bilioni 164.86 zinahitajika. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea imetenga jumla ya kiasi cha shilingi 31,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maabara katika Kituo cha Afya cha Mjimwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza.

MHE. MARIAMU M. NYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Swali la kwanza; kwa kuwa kituo hiki ni muhimu kwa wananchi wa Kata ya Mjimwema pamoja na wananchi wote wa Manispaa ya Songea; nini sasa mkakati wa Serikali wa kukarabati kituo hiki ikiwa ni pamoja na miundombinu pamoja na majengo yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi ya wanaume pamoja na wanawake katika kituo hiki? Ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninajibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Nyoka, Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia halmashauri tumeanza kwa kutenga hiyo shilingi 31,000,000 lakini kama haitoshi tutakwenda kufanya ufuatiliaji na ninamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri aandike andiko ambalo litakuja Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tuone maoteo ya fedha tuliyonayo katika bajeti zetu ili tuhakikishe kwamba tunaendelea kuboresha miundombinu katika kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na kujenga wodi ya wanaume na wanawake sambamba na lile swali dogo la kwanza ambalo nilijibu, vilevile ninamwelekeza Mkurugenzi ashirikiane na *DMO* waweze kutuandikia andiko Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili na sisi tuweze kutoa maelekezo ya namna ya kuanza ujenzi wa wodi hizo za wanaume na wanawake wapate huduma katika kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy Kombani, swali la nyongeza.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Kijiji cha Kichangani katika Jimbo la Ulanga wameonyesha utayari wa kushirikiana na Serikali ambapo wamejenga jengo la kliniki ya mama na mtoto na wamefikia hatua ya kupaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupata kauli ya Serikali, je, ni lini itakuwa tayari kuwa-*support* hawa wananchi kwa kutenga fedha ili kumalizia kile kituo ili juhudi zao zisipotee na hizi huduma za mama na mtoto ziweze kuanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Kombani kama alivyoliuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapongeza juhudi za wananchi ambao tayari wameshaanza kujenga jengo hili na limefika *level* ya *lintel*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaendelea kutenga fedha kukamilisha vituo hivi na tumeanza na vile vituo vya afya 111 ambapo bajeti yake nimekwishaisema. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumechukua kama ombi ili Ofisi ya Waziri Mkuu,

TAMISEMI tuweze kulifanyia kazi na kutengea bajeti ya kukamilisha miundombinu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Isack Joseph, swali la nyongeza.

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka mara ya mwisho niliripoti kuhusu zahanati yangu ya Ngaruka iliyopata hitilafu ya kuungua na akatoa maelekezo kwamba angalau halmashauri ianze kazi ya kukarabati. Je, ni lini Serikali itapeleka vifaatiba kwenye zahanati hiyo kwa kuwa tayari halmashauri imeshafanya hatua ile ya awali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninampongeza Mheshimiwa Isack Joseph kwa sababu zahanati hii aliwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kama mpango wa dharura na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tukatoa maelekezo kwa halmashauri ifanye ukarabati wa haraka ili wananchi waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye eneo la vifaatiba ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tumepokea, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itahakikisha kwamba sasa tunafanya mawasiliano ya ndani na *MSD* kuhakikisha kwamba vifaatiba vinakwenda kwenye zanati hii na viweze kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Marirta Gido, swali la nyongeza.

MHE. MARIRTA G. KIVUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itajenga wodi ya mama na mtoto katika Kituo cha Afya Malambo, Wilayani Ngorongoro?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama ambavyo nimeshatoa majibu kwenye jibu la msingi na maswali mengine madogo ya nyongeza, ninamhakikishia Mheshimiwa Gido, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaendelea kuratibu na kuhakikisha kwamba tunafanya ufuatiliaji na ukamilishaji wa majengo haya ya mama na mtoto, zile wodi za mama na mtoto, kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia hili na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaendelea kuratibu na kuhakikisha kwamba kadiri bajeti inavyoruhusu tunapeleka fedha katika maeneo haya ili kukamilisha miundombinu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Japhael Lufungija, swali la nyongeza.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Ninataka niulize; Jimbo la Ulyankulu linavyo Vituo vya Afya vya Mgerela ambako Serikali ilitupa fedha, Kituo cha Afya cha Ulyankulu, Ilege, Kashishi pamoja na Mwongozo na Uyowa, lakini vituo vya afya vya Mgerela, Ilege na Kashishi havina wodi za watoto. Sasa, ni lini Serikali itatupa fedha ili kuweza kujenga wodi za watoto katika vituo hivi vya afya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lufungija, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri akishirikiana na Mganga Mkuu wa Halmashauri walete andiko Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuonyesha uhitaji wa wodi hizi za watoto katika maeneo haya ili tuanze kutenga fedha na kuhakikisha kwamba tunazijenga, zikalete huduma bora kwa wananchi hawa wa Ulyankulu na Mheshimiwa Mbunge apeleke tabasamu kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Lukumay, swali la nyongeza.

MHE. JOHANNES L. LUKUMAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Serikali. Mpango wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kwamba kila kata katika nchi hii ipate kituo cha afya. Jimbo la Arumeru Magharibi lina kata 27, lakini lina vituo nane tu vya afya. Je, Serikali itajenga lini vituo vya afya vitano, kwa miaka mitano kuanzia hivi sasa katika Kata za Sambasha, Kimnyak, Bangata, Musa na Kiranyi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Lukumay kama ambavyo ameliuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mpango wa Serikali ni kujenga vituo vya afya kila kata. Kwa sasa tunaelekea kwenye zile kata za kimkakati, zenye vipaumbele, zenye idadi kubwa za

wananchi. Kwa sababu zipo kata ambazo ukijenga zahanati inakidhi kutoa huduma. Kwa hiyo, kama utajenga kituo cha afya kwenye kata jirani wale wananchi wanakuwa wanapata *referral* kwenda kupata matibabu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Dkt. Lukumay pamoja na Wabunge wote kwamba mpango wa Serikali ni kujenga vituo vya afya kila kata, lakini tutaanza na zile kata za kimkakati hasa zenye idadi kubwa ya wananchi ili kuhakikisha kwamba zinatoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Dkt. Lukumay, pamoja na wananchi anaowaongoza, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaendelea kuratibu hili na kuhakikisha kwamba tunajenga vituo hivi vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 46

Uhitaji wa Kidato cha Tano na Sita Shule ya Sekondari Ngara Mjini

MHE. DOTTO J. BAHEMU aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Ngara Mjini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Mbunge wa jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikijenga shule mpya za kidato cha tano na sita au kuongeza miundombinu katika shule za sekondari zilizopo ili kuzipandisha hadhi kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 hadi 2025/2026, Serikali imepeleka shilingi bilioni 2.08 katika Halmashauri ya Ngara kwa ajili ya kuongeza miundombinu katika Shule saba za Sekondari za Rusumo, Kabanga, Lukole, Muyenzi, Murugamba, Ndomba na Ngara *High School* na kuzipandisha hadhi ambapo kwa sasa zina jumla ya wanafunzi 6,881 wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Shule ya Sekondari ya Ngara Mjini, shule hii kwa sasa haina mahitaji makubwa ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Shule ya Sekondari Ngara Mjini ipo katika Tarafa ya Nyamiaga yenye shule tatu za kidato cha tano na sita ambazo ni Rusumo, Lukole na Ngara *High School* zenye jumla ya wanafunzi 2,915. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa miundombinu ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita kwa kuzingatia tathmini ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, swali la nyongeza.

MHE. DOTTO J. BAHEMU: Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Serikali ni majibu ambayo yanatuvunja moyo sisi wananchi wa Jimbo la Ngara. Kusema kwamba kwa sasa Shule ya Sekondari ya Ngara Mjini haina uhitaji maana yake ni kwamba Serikali haina mpango wa kuweka kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa Wananchi wa Ngara wanojibiwa hivi ndiyo ambao walimpigia kura nyingi sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wakitegemea haya ambayo tunayaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Ngara Mjini ni shule ambayo iko katikati ya makao makuu ya wilaya na ule Mji wa Ngara ndiyo ambao unaongoza sasa hivi kwa kuwa na kiwango kikubwa sana cha uzalishaji wa *population* katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba, kuna haja ya kufanya tathmini upya kulingana na jinsi ongezeko la watu ili kuangalia namna gani ambavyo sasa tunaweza tukapata kidato cha tano na cha sita kwa kuzingatia kwamba tunao Mradi mkubwa wa Tembo *Nickel* ambao unakuja, ambao utakuwa na watu wengi ambao wategemezi wao watakuwa wanakaa katika ule Mji wa Ngara. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika halmashauri zenye shule nyingi za kidato cha tano hapa nchini, Halmashauri ya Ngara ina shule tisa za kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka miwili ya fedha 2024/2025 na 2025/2026 tu, ndani ya miaka miwili, imejengewa shule saba za kidato cha tano na sita. Shule hii ya Sekondari Ngara Mjini ambayo iko ndani ya Tarafa ya Nyamiaga, tarafa moja ina shule tatu za kidato cha tano na sita. Kwa hiyo, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge, nchi hii ni kubwa na mahitaji ni makubwa, tunajali mahitaji ya Ngara, tunaangalia takwimu za wanafunzi na tunaangalia *catchment population* ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Shule ya Sekondari ya Ngara Mjini inazungukwa na shule tatu za kidato cha tano na sita ndani ya tarafa moja na haina uhitaji mkubwa wa kupeleka shule kidato cha tano na sita. Ninakubaliana na Mbunge kwamba huko mbele tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu kwa kadiri mahitaji yatakavyoongezeka ili shule hii na yenyewe iweze kupata sifa ya kupata kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John Luhende, swali la nyongeza.

MHE. JOHN S. LUHENDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Jimbo la Bukene ni jimbo lenye kata 17 lakini ni jimbo ambalo halina shule hata moja ya kidato cha tano na cha sita. Swali langu ni kwamba; ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ujenzi wa shule ya sekondari ya kidato cha tano na cha sita?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bukene na ni kweli kwamba moja ya hoja ambayo ameleta mara kadhaa katika Ofisi Waziri Mkuu, TAMISEMI ni kuomba ujenzi wa shule za Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari Serikali tumeshafanya tathmini katika Jimbo la Bukene, kwa kushirikiana na halmashauri tumeshaainisha shule na maeneo ambayo tunahitaji kuongeza madarasa ya Kidato cha Tano na Sita na tupo kwenye taratibu za kibajeti na mara baada ya taratibu hizo kukamilika, ninamthibitishia Mbunge kuwa, tutapeleka fedha kwa ajili ya kujenga madarasa ya kidato cha tano na sita pamoja na mabweni ili wanafunzi wa Bukene wapate mazingira bora zaidi ya elimu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cornel Magembe, swali la nyongeza.

MHE. CORNEL L. MAGEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Chato Kaskazini tuna Kata inaitwa Kigongo ambayo idadi ya watu ni zaidi ya 63,000, lakini kwa sababu ya ongezeko kubwa la watu na kuzaliana kwa wingi tumejitahidi katika kata hiyo kujenga shule za sekondari tano mpaka sasa kwenye kata moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika kata hii, katika vijiji vyote na shule zile tano, hatuna shule ya kidato cha tano na sita. Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba, wakati umefika sasa wa kuifanya Shule ya Sekondari Kigongo iliyopo katika Kata ya Kigongo kuwa *high school* ili iweze kusaidia wale watoto wanaotoka katika shule zile tano katika kata ile moja na zaidi ya watu 63,000 ambao wanaishi hapo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Cornel Magembe, Mbunge wa Jimbo la Chato Kaskazini na ninawapongeza sana Halmashauri ya Chato kwa kujenga shule tano ndani ya Kata ya Kigongo na hiyo ni kuwathamini wanafunzi wetu kwa kuwawezesha kupata fursa nzuri za masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, moja ya dhamira ya Serikali ni kuhakikisha katika maeneo yote yenye sifa ya kupata shule za Kidato cha Tano na Sita, tunaainisha maeneo, tunatenga bajeti na kujenga madarasa na mabweni ili wanafunzi wapate ukaribu na ubora wa elimu katika mazingira yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge na wataalamu wake watuletee pendekezo la kata ambayo ina shule ya sekondari

yenye eneo la kutosha kwa ajili ya kuongeza madarasa ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, katika Kata ya Kigongo, lakini kwa kadiri watakavyokubaliana kama halmashauri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutapokea kwa ajili ya hatua zaidi ili tujenge shule ya kidato cha tano kulingana na vigezo na wanafunzi wetu wapate mazingira bora zaidi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 47

Ujenzi wa Soko la Kisasa Halmashauri ya Mji wa Mbulu

MHE. YUSTINA A. RAHHI aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Soko la Kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na soko la kisasa katika Mji wa Mbulu. Kwa kuzingatia umuhimu huo, mradi huu ni miongoni mwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji na Halmashauri nchini *(TACTIC)* Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na, Halmashauri ya Mji wa Mbulu kutenga eneo la ujenzi na taratibu zote za umiliki wa ardhi kwa ajili ya mradi huo. Aidha, tayari upembuzi yakinifu, usanifu wa kina wa majengo na gharama za mradi zimejulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaanza ujenzi pindi taratibu za kibajeti zitakapokamilika na zabuni kutangazwa kuwapata wakandarasi na washauri elekezi kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yustina, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imeelekeza ujenzi wa soko la kisasa katika Mji wa Mbulu kutekelezwa katika mpango wa *TACTIC*. Sasa hii inayoitwa awamu ya tatu ni lini itaanza kutekelezwa? Ukizingatia wananchi wa Mbulu wamekuwa wakisubiria Mradi ya *TACTIC* kwa muda mrefu kwa kuwa una vipengele vya ujenzi wa stendi, dampo pamoja na lami katika Mji wa Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameshajitolea maeneo kama stendi yamekwishapatikana, sasa watarajie lini *TACTIC* inakwenda kutekelezwa katika Mji wa Mbulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; ili kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogo wadogo, Serikali imetoa agizo kwamba, halmashauri zote nchini zitenge asilimia tano ili kusaidia kuboresha wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Manyara wajasiriamali katika miji midogo midogo ambayo nyingine tunaita vijiwe, hasa wafanyabiashara wa mboga mboga na matunda, utaona wametandika bidhaa zao chini ili waweze kuuza. Sasa, ni

lini halmashauri zitaanza kusaidia wafanyabiashara hao wadogo wadogo hata angalau kwa kujenga paa ili wafanyabiashara hawa wasiathirike na mvua na jua? Ahsante? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Yustina Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara. Kwa kweli amekuwa mchapakazi na msemaji mahiri sana wa wananchi wa Mkoa wa Manyara na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Mji wa Mbulu iko kwenye Mradi wa Uboreshaji Miji, *TACTIC* ya Awamu ya Tatu na katika kundi hili zipo halmashauri 18. Katika halmashauri hizi 18 Halmashauri ya Mbulu itajengewa soko la kisasa, stendi ya mabasi ya kisasa pamoja na barabara za lami kilometa 3.6 na tayari tuko hatua nzuri. Kwanza, tumeshaandaa *document* za zabuni pia tumeshafanya usanifu na upembuzi wa kina, taarifa zote tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua inayoendelea hivi sasa ni Serikali pamoja na wadau wa maendeleo kwa maana Benki ya Dunia tuko kwenye majadiliano ya mwisho wakati tunakamilisha miradi ya awamu ya kwanza na ya pili ambayo ilihusisha majiji na manispaa. Tuko hatua za mwisho sana, baada ya hapo tutakwenda kwenye hatua ya utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu katika halmashauri za miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Rahhi kwamba wananchi wa Mbulu Mjini wapo katika mikono salama ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na tutahakikisha kwamba mradi huo unatekelezwa na kuboresha Mji wa Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kweli Serikali kwa kuthamini mazingira ya masoko katika miji yetu; wananchi wetu

wamekuwa wanafanya biashara katika mazingira magumu, katika mazingira ya jua, mvua na kadhalika na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu, Serikali ilishatoa maelekezo kwamba kila halmashauri lazima itenge fedha za mapato ya ndani yasiyolindwa, asilimia tano ya yale mapato, kwa ajili ya maboresho masoko ya wajasiriamali wadogo wadogo na tayari utekelezaji wa maelekezo haya umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika pale Dar es Salaam, Manispaa ya Ubungo, Kinondoni, Temeke na baadhi ya miji hapa nchini utakuta kuna vibanda vizuri sana vidogo vidogo vya biashara vinajengwa kwa ajili ya wananchi kupata nafasi ya kufanya biashara. Kwa wale ambao watakwenda Dar es Salaam ukipita Magufuli *Terminal* eneo lile lote lina vibanda vizuri sana vinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na tutaendelea kusimamia hilo na ninatoa wito kwa Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanatekeleza maelekezo hayo kwa kujenga mazingira bora ya biashara kwa wafanyabiashara. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge wa Ilongero, sasa aulize swali lake.

Na. 48

Ujenzi wa Barabara ya Lami Kutoka *TRA* – Njia panda Manyara

MHE. HAIDERALI H. GULAMALI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya kutoka *TRA* - Kinyeto - Merya hadi Njia panda Manyara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Ilongero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya *TRA* – Kinyeto – Merya hadi Njia panda ya Manyara ina urefu wa kilometa 52.4, kati ya hizo kilometa 3.4 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 49.0 ni za udongo na changarawe. Barabara hii ni muhimu kwa kuwa ni njia muhimu katika shughuli za kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Halmashauri ya Wilaya ya Singida na imekuwa mbadala wa Barabara Kuu ya Singida – Manyara. Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini imekuwa ikifanya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ilitumia shilingi milioni 180.19 kwa ajili ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara hii na katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 442.11 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Barabara ya *TRA* – Kinyeto – Merya hadi Njiapanda ya Manyara ili iweze kupitika na kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mipango ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa hatua mbili yaani kufanya usanifu na baadaye kutafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haiderali Hussein, swali la nyongeza.

MHE. HAIDERALI H. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza; Mheshimiwa Naibu Waziri ametuambia kwamba shilingi 180,000,000 zilitumika kujenga kilometa 3.4 kwa mwaka 2024/2025 na sasa anadai shilingi

440,000,000 kwa ajili ya msimu huu wa 2026/2027. Je, fedha hizo zitaenda kujenga kilometa ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Naibu Waziri amekiri kilometa 49, sasa kwa mwendo huu kwa kweli anataka kutuma ujumbe kwa wananchi wa Singida kwamba miaka 20 ijayo ndiyo barabara hiyo itakamilika? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge bingwa kabisa wa Jimbo la Ilongero kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya kuwasemea wananchi wa Jimbo hilo. Pili, nimhakikishie tu kwamba tunatambua kwamba barabara hii ni barabara muhimu sana na ni barabara ambayo ina uhitaji wa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, kila mwaka wa fedha tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya kuihudumia barabara hiyo. Tumepeleka shilingi 180,000,000 mwaka wa fedha uliopita, mwaka huu tumepeleka shilingi 442,000,000 kwa ajili ya kuiboresha iweze kupitika kwa kiwango cha changarawe kilichopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo, katika bajeti hii hii pia ipo fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa ajili sasa ya kuwa na bajeti ya jumla ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ambapo sasa baada ya kupata gharama halisi tutaanza kutenga fedha kwenye bajeti zetu kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo kwa awamu kwa vipande vya lami mpaka kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hatutarajii kwamba tutakwenda miaka 20. Serikali hii haijawahi kujenga barabara moja kwa miaka 20 na

tutaendelea kutenga bajeti. Ni muhimu tuhakikishe kwamba barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fadhili Ngajiro, swali la nyongeza.

MHE. FADHILI F. NGAJILO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi iliniulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Iringa Mjini lina barabara takriban kilometa 49 ambazo zimejengwa, tunaishukuru sana Serikali; hiyo ni sawa na asilimia 9.2. Hata hivyo, ule mji unakuwa kwa kasi sana na barabara nyingi ni mbovu, hazipitiki. Barabara kama za Kitasengwa – Mkola – Nduli; Kihongolelo – Mafifi – Kihesa; Majitaka - Don Bosco – Bombambili – Mawelewele – Lugenge – Kwakabali; na Makorongoni – Ilala – Kitwiru – Igumbilo; kote kuna barabara ambazo hazipitiki. Sasa swali; je, ni lini Serikali itatuongezea fedha ya bajeti Jimbo la Iringa Mjini ili tuweze kuzijenga barabara hizi kwa kiwango kizuri cha lami, ili mji ule uweze kuwa mji mzuri wa biashara na utalii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, Mheshimiwa Fadhili Ngajilo na nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwasemea wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Naibu Spika, wiki moja iliyopita tulifanya ziara pale, mimi pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya *LAAC* na tulikagua miradi ya maendeleo katika Manispaa ya Iringa, ikiwemo ujenzi wa barabara za kiwango cha lami ambazo zinajengwa kupitia Mradi wa *TACTIC* awamu ya pili. Kwa kuanza, niwapongeze wananchi wa Iringa Mjini na Mheshimiwa Mbunge kwa kupata mradi wa awamu ya pili ambao utekelezaji wake unaendelea vizuri; na tulisisitiza kwamba barabara zile zikamilike. Miongoni mwa barabara ni hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili; tunatambua kwamba ziko barabara ambazo zinahitaji matengenezo. Tayari tumeshatoa maelekezo kwa Mameneja wote wa *TARURA* mikoa na wilaya kuainisha barabara zote korofi na kuleta maombi maalum ambayo tutayapeleka nje ya bajeti kuhakikisha kwamba tunarekebisha maeneo ambayo ni *critical* kwa ajili ya kuwezesha wananchi kusafiri. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutalifanyia kazi hilo na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunazifanyia matengenezo barabara zote ambazo amezitaja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Makanya kwenda kwenye machimbo ya *Gypsum* ni barabara ambayo inachochea sana uchumi wa Halmashauri ya Same na pia inaongeza kipato kwa wanawake ambao wanachimba madini hayo katika maeneo hayo, lakini barabara hii haipitiki kipindi cha mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika kipindi chote cha mvua?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kilimanjaro, mama yangu Mheshimiwa Zuena Bushiri kwa uchapakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu kuwa, kuna uhitaji mkubwa sana wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Safari ni hatua, tunakwenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba barabara hizi ambazo zinatumika na wananchi wetu kwenda kwenye shughuli za kijamii na kiuchumi kwa ukubwa

wake tunatenga fedha na kuhakikisha kwamba zinapitika msimu mzima wa mwaka mzima. Kwa hiyo ninaomba nitumie nafasi hii nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Same, wafike kwenye barabara hii ya Makanya kuelekea machimbo kufanyia tathmini maeneo yote korofi na nini kinaweza kikafanyika ili Serikali iweze kupeleka fedha kwa ajili ya kuirekebisha barabara hiyo na wananchi wanaofanya shughuli za uchimbaji wa madini waweze kufanya shughuli zao kwa ufasaha zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Utaly, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Katika Jimbo la Lindi Mjini, Kata ya Tandangongoro, tunayo Barabara ya Mtutu – Cheleweni. Barabara hii inapita katika maeneo ya Nandambi na Mkanga na umuhimu wa barabara hii ni kuwa maeneo haya ndiko ambako kunazalishwa korosho kwa wingi, ufuta pamoja na mahindi. Hata hivyo, barabara hii imekuwa mbovu na haipitiki kwa sasa. Je, ni lini Serikali itafanya matengenezo ya kina ya barabara hii ili iweze kupitika katika vipindi vyote vya mwaka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na pia nimpongeze Mheshimiwa Mohamed Utaly, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini kwa kazi nzuri kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao uhakika kwamba kwa kupitia maelekezo ya Serikali 60% ya zabuni za bajeti ya mwaka huu wa fedha 2026/2027, zimetangazwa na maeneo mbalimbali tunao makandarasi na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha miezi mitatu, Serikali imekwishapeleka zaidi ya shilingi 150,000,000,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini ikiwemo katika Manispaa ya Lindi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Ninatambua changamoto ya barabara katika Kata ya Tandangongoro, lakini pia ninafahamu kwamba barabara hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ya Mtutu – Cheleweni ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikuhakikishie tu, tutafuatilia baada ya hapa; kama si miongoni mwa barabara ambazo zimetangazwa kwa 60% ambazo tayari zinaendelea na hatua za zabuni, tutafanya utaratibu wa haraka kuhakikisha kwamba barabara hii na yenyewe inatangazwa na kupata wazabuni kwa ajili ya kufanya marekebisho ili iweze kupitika vizuri.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata. Swali la Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako.

Na. 49

Ujenzi wa Barabara ya Mugombe - Kagerankanda

MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO K.n.y. MHE. EDIBILY K. KINYOMA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mugombe – Kagera Nkanda ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Edibily Kinyoma Kazala, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 89.4 kwa ajili kufanya matengenezo ya kawaida na usanifu wa ujenzi wa Barabara ya Mugombe - Kagerankanda, yenye urefu wa kilometa 37, ili kupata gharama halisi za ujenzi wake. Baada ya kubaini gharama hizo, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026, barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo ya urefu wa kilometa 19 kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya Shilingi milioni 534.26. Serikali itaendelea kuiboresha barabara hii kwa tabaka la changarawe ili iweze kupitika misimu yote wakati maandalizi ya usanifu wa barabara hiyo yakiendelea. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, swali la nyongeza.

MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba kwa sasa mvua zimeshaanza kunyesha kule Kasulu na barabara hii ya Mugombe – Kagerankanda hali yake si nzuri. Tunatambua mipango ya Serikali iliyopo, lakini kwa kuzingatia kwamba kuna tishio kubwa la *El Niño*. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kutafuta fedha za dharura ili kutengeneza barabara hiyo ili iweze kupitika hata wakati wa mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; katika Jimbo la Kasulu Mjini, Barabara ya Kasulu – Kabanga – Bugaga; na Barabara ya Mwanga – Msambara zina hali mbaya sana na Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu, kwamba tayari tumeomba barabara hizo zitengenezwe kwa utaratibu wa dharura. Je, ni lini Serikali itatoa fedha hizo ili barabara hizo ziweze kutengenezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa

Naibu Spika, ahsante sana. Nitumie nafasi hii nimpongeze sana mama yangu, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, mchapakazi kabisa, Mbunge wa Kasulu Mjini, kwa kuwasemea wananchi wa Kasulu Mjini na hoja kadhaa amezileta kuhusiana na barabara lakini na masuala mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Barabara hii ya Mugombe – Kagerankanda ni barabara muhimu. Nimthibitishie tu kwamba, pamoja na kwamba mwaka wa fedha uliopita ilitengenezwa kwa gharama ya zaidi ya shilingi 534,000,000, lakini mwaka huu wa fedha 2026/2027, imetengwa shilingi milioni 89.4, tayari zipo kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii sasa nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kigoma pamoja na Wilaya ya Kasulu wafike kwenye barabara hiyo ili waone uwezekano wa ile 60% kuhusisha barabara hii kutokana na umuhimu wake kabla ya msimu wa mvua ili wananchi waweze kupita vizuri; kwa sababu bajeti ipo, hivyo ni suala lao kuamua kuipa kipaumbele kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Barabara ya Kasulu – Kabanga – Bugaga na barabara nyingine ambazo Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu Mjini amezisema ni miongoni mwa barabara muhimu na Serikali inatambua hilo na tumeendelea kuzitengea bajeti. Tunafahamu udharura wake. Ninaomba tu nimthibitishie kwamba tutajiridhisha, kama barabara hizi haziko kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha, tuone namna nzuri ya kuzitafutia fedha kwa taratibu za kidharura kutokana na umuhimu wake kwa kadiri ya tathmini ili barabara hizo nazo ziweze kupitika. Kama barabaara hizi ziko kwenye bajeti, basi tutazipa kipaumbele ili ziweze kutengenezwa na wananchi waweze kupita kwa ubora zaidi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Alan Mvano, swali la nyongeza.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. katika Wilaya ya Kakonko wapo wananchi wanaoishi katika Kata ya Nyamtukuza maeneo ya

Nyamirongo, Lutenga na Kavungwe, ambao wanalazimika kutembea kilometa 90 hadi 100 kufika kufika makao makuu ya wilaya kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika mbadala wake, tunayo barabara ambayo ni ya kilometa 55 tu, ambayo tayari Serikali imekwishaifungua kwa kilometa 35; zimebakia kilometa 20 kupitia Katengera na Bwera ili wananchi wa kutokea maeneo yale, badala ya kutembea kilometa 90 hadi 100, basi waweze kutembea kilometa 55, kufika makao makuu ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; je, ni lini Serikali sasa itafungua hizo kilometa 20 na ikiwezekana kwa kutumia fedha hizi za dharura za *El Nino* ili msimu huu wa mvua unaoendelea basi wananchi hawa waweze kupata huduma ya barabara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kakonko, Mheshimiwa Alan Mvano na nimpongeze kwa namna ambavyo anawapambania wananchi wa Jimbo la Kakonko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, moja ya vipaumbele vya Serikali ni kurahisisha mawasiliano ya barabara kwa wananchi; wananchi wanaotoka pembezoni mwa halmashauri kwenda makao makuu ya halmashauri, lengo ni kurahisisha. Kama kuna barabara fupi zaidi ambayo itaokoa gharama za usafiri, basi ni kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kuwa hii barabara ambayo ameitaja, ya Katengera – Bwera na kwenda makao makuu ni barabara ya *shortcut* ya kilometa 55 badala ya ile ndefu ya kilomita 90, ninaomba nitumie nafasi hii nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kigoma pamoja na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Kakonko, kwanza wafanye tathmini ikiwa imekwishasajiliwa kwenye mtandao wa barabara za *TARURA*.

Ikiwa haijasajiliwa, walete maombi kwa haraka ili iweze kusajiliwa kuwa barabara rasmi ya *TARURA* na iweze kufunguliwa kwa taratibu zetu za kibajeti ili iweze ku-*save purpose* ya kupunguza umbali kwa wananchi wa Kakonko.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, swali la nyongeza.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Jimbo la Kalambo katika Kata ya Mpombwe kuna kijiji ambacho kiko mipakani mwa Zambia na Tanzania. Niliwahi kuuliza swali na Waziri akanijibu kwamba barabara ile haijasajiliwa. Niombe sasa Serikali kutoka pale makao makuu ya kata kwenda kule Kijiji cha Chipwa, ni kilometa 6.8, hawajawahi kuona barabara toka kupata uhuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga barabara hiyo ili wananchi hao waweze kupata huduma kama wananchi wengine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na nimpongeze Mheshimiwa Edifonsi Kanoni, Mbunge wa Jimbo la Kalambo kwa ufuatiliaji na ni kweli kwamba tumeshakaa mimi na yeye mara kadhaa kuhusiana na barabara hii, ni barabara muhimu. Ninaomba tu nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, jambo la kwanza ambalo Serikali inalifanya siku zote ni kuhakikisha kwamba barabara zile muhimu kwa wananchi zinapewa kipaumbele. Barabara hizi zinatakiwa ziibuliwe kuanzia ngazi ya halmashauri, zile ambazo bado hazijasajiliwa kwenye mtandao wa *TARURA*, baada ya hapo sasa Serikali kupitia *TARURA* itaanza kutenga bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameongelea barabara hii kutoka Makao Makuu - Chipwa, kwamba ni barabara ambayo haijawahi kujengwa, maana yake ni barabara ambayo haipo kwenye mtandao wa *TARURA*. Kwa hivyo, ninaomba nitumie nafasi hii nimwelekeze Meneja wa

TARURA wa Mkoa wa Rukwa pamoja na Wilaya ya Kalambo, waifanyie tathmini barabara hii, wafuate taratibu za kusajili barabara hii ili iweze kuingia kwenye mtandao wa *TARURA* na baada ya hapo Serikali sasa itatenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inafungua barabara hii na kuendelea kuijenga mara kwa mara ili kusogeza huduma za usafiri kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 50

Ukuzaji wa Sekta Binafsi ili Kuongeza Ajira

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE K.n.y. MHE. DKT. REGINA C. MALIMA aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha inaimarisha mazingira ya uzalishaji na ukuaji wa Sekta binafsi inayobeba ajira nyingi kwa Vijana?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chaya, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa sekta binafsi katika kuongeza uzalishaji, uwekezaji na ajira kwa vijana. Katika kutekeleza Dira 2050, Serikali imeandaa Mkakati wa

Taifa wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (*MKUMBI II)*, unaolenga kupunguza gharama za kufanya biashara, kurahisisha taratibu za uwekezaji na kuimarisha mazingira ya uzalishaji na utoaji wa huduma. Pia Serikali imesaini Azimio la pamoja kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma la 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa *MKUMBI One* ya mwaka 2024, Tathmini ya Sekta Binafsi ya mwaka 2024 na Taarifa ya Hali ya Sekta Binafsi Tanzania ya mwaka 2026 zimebainisha mwenendo, changamoto na fursa za sekta binafsi nchini. Kwa kuzingatia matokeo na mapendekezo ya taarifa hizo, Serikali imeanza maandalizi ya kuandaa Sheria ya Maendeleo ya Sekta Binafsi, inayolenga kuimarisha uratibu wa taasisi za sekta binafsi, ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi, pamoja na utawala bora ndani ya taasisi za sekta binafsi. Aidha, Serikali itaweka mfumo wa kushughulikia changamoto zinazoathiri uzalishaji, uwekezaji na ukuaji wa biashara kuanzia ngazi ya Kitaifa hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inaendelea kuimarisha majukwaa ya majadiliano na sekta binafsi pamoja na Idara za Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika ngazi za mikoa na wilaya. Aidha, imeandaa kipimo cha ushindani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (*LGA Business and Investment Competitiveness Index*) ili kuchochea utoaji huduma kwa wafanyabiashara na wawekezaji. Hatua hizi zinalenga kuongeza uzalishaji, ushindani wa biashara za ndani na uwekezaji unaopanua fursa za ujasiriamali na ajira zenye tija kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy Mwakyembe, swali la nyongeza.

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pia, napenda kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Ninaomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, changamoto ya ajira kwa vijana ni kubwa nchini. Je, mkakati huu unaanza lini, ili kuleta matunda, kwa ajili ya vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nini matarajio ya ndani ya muda mfupi, mpango huu kuweza kufanya kazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Lucy Mwakiembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Lucy Mwakyembe, na vilevile Mheshimiwa Dkt. Regina Malima. Mara nyingi wamekuwa wanachangia sana suala la ajira, hususan, utetezi wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kujibu swali la kwanza, kuhusu mkakati wa *MKUMBI II,* utaanza lini; tayari tumeandaa ule mkakati na tayari tumeuwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri, kwa ajili ya kupitishwa. Kwa hiyo, wakati wowote ule, Baraza la Mawaziri likiupitisha, mkakati ule wa *MKUMBI II,* utaanza kufanya kazi, na tutazitaarifu Wizara, taasisi na Serikali za Mitaa ni namna gani tunaenda kuanza kuutekeleza mkakati ule wa *MKUMBI II*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, je, tunategemea matarajio gani ndani ya muda wa kati na muda mfupi wa huu mkakati; kwenye mpango wetu wa miaka mitano, huu wa nne, tumeweka matarajio ya kutengeneza ajira milioni nane. Kama unavyofahamu, sekta binafsi imepewa 70% ichangie kwenye Pato la Taifa, lakini hiyohiyo 70% inatakiwa ichangie kwenye ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mategemeo yetu ni tutakapoboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, tunategemea kupokea wawekezaji wengi zaidi. Tunategemea ile

sekta binafsi, isiyo rasmi, iwe rasmi, ili watu waweze kuajiri vijana wengi, lakini watoe ajira zenye staha. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumejipanga, kama Serikali, na ndani ya muda mfupi tukianza utekelezaji wa *MKUMBI II,* tunategemea kutengeneza ajira nyingi sana. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Arif Suleiman, swali la nyongeza!

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tunazungumzia sekta binafsi na ajira kwa vijana:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa karibuni Serikali, kule Kusini, iligundua gesi takribani futi za ujazo, bilioni 223, lakini kuna malalamiko mengi sana kutoka Mkoa wa Mtwara, hususan kuhusiana na ajira! Kwamba, chanzo hicho cha nishati kinatumika, kwa ajili ya viwanda ambavyo vipo katika mikoa mingine. Je, Serikali imejipanga vipi kuhamasisha kuhusiana na uwekezaji wa viwanda katika Mkoa wa Mtwara, Jimbo la Mtwara Vijijini, ili vijana wa Mkoa wa Mtwara, na Jimbo la Mtwara Vijijini waweze kupata ajira?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Arif, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa maswali yake. Amekuwa anauliza sana suala la, ni jinsi gani Serikali imejipanga kuvutia wawekezaji, hususan uwekezaji wa viwanda vya mbolea, na wawekezaji wa viwanda vingine Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati, tumekuwa tunashirikiana katika kutafuta wawekezaji, hususan kwenye gesi. Hivi karibuni, kama mnatambua, mlimuona Waziri wa Nishati ametoa taarifa ya kwamba, tunaelekea kuzuri, kwanza katika vile visima ambavyo tunavichimba, na vilevile tunaendelea kutafuta wawekezaji wa gesi kwa kutumia mfumo wa ubia, *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mtwara ni mojawapo ya mikoa ya kipaumbele ukizingatia kwamba, ile sheria yetu na mkakati wa *local content* unataka wanufaikaji wa kwanza wa rasilimali za nchi wawe wananchi wa kutoka maeneo yale. Kwa hiyo, na sisi tunapozunguka huko duniani kutafuta wawekezaji, hususan wale wanaoenda kutumia rasilimali ya gesi, kipaumbele tunapeleka kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara; ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali, ushauri wake vilevile tumeupokea.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea; Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake!

Na. 51

Kuwezesha Vijana Nchini

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka 4% au 10% kwa kila Wizara ya Kisekta, kwa ajili ya kuwawezesha vijana?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa, uwezeshaji wa vijana ni jukumu mtambuka linalohitaji ushiriki wa Wizara zote za Kisekta kulingana na majukumu na fursa zilizopo katika sekta husika. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali,

kupitia Wizara mbalimbali, imetumia kiasi cha shilingi bilioni 966.8, kwa ajili ya programu na shughuli za uwezeshaji vijana zilizowafikia vijana 6,933,835. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imepanga kutumia takribani shilingi trilioni 1.853, kwa ajili ya kuwawezesha vijana 18,644,433. Hatua hizi zinaonesha dhamira ya Serikali kuendelea kutenga rasilimali, kwa ajili ya maendeleo na uwezeshaji wa vijana kupitia sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapokea pendekezo la kutenga asilimia nne au 10 ya bajeti ya kila Wizara ya Kisekta, kwa ajili ya uwezeshaji vijana, na italitathmini katika muktadha wa maandalizi ya mipango na bajeti za Serikali kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa, majukumu ya kisekta, na upatikanaji wa rasilimali. Lengo ni kuhakikisha vijana wanapata fursa stahiki na kunufaika na programu za Serikali kwa kuzingatia vigezo na taratibu zilizowekwa. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juwakali, swali la nyongeza!

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo mazuri, lakini nina swali na ushauri mmoja:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ataungana na mimi kwamba, huwezi kuzungumza fursa za uwezeshaji za vijana, usiiguse Wizara ya Kisekta. Unapozungumzia Wizara ya Madini, lazima utawakuta vijana, utakapozungumzia Wizara ya Uwezeshaji utawakuta vijana, vilevile utakapozungumzia Wizara ya Viwanda na Biashara utawakuta vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo utaungana na mimi kwamba, Wizara nyingi za Kisekta matokeo yake yawafikie au yananatakiwa yawafikie vijana! Mheshimiwa Waziri ninataka kufahamu, hamuoni sasa umefika wakati wa kuleta sheria maalum Bungeni, ili tuone kwamba, mapendekezo ambayo yanapendekezwa, na fursa zinazotoka katika Wizara za Kisekta ziwe ni sheria maalum, kwa ajili ya kuwasaidia vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu; Mheshimiwa Waziri utaungana na mimi, na Wabunge wenzangu wataungana na mimi kwamba, kwenye Wizara hizi za Kisekta hakuna mwongozo wowote. Kama hakuna mwongozo wowote, kutakuwa hakuna *expectations* ambazo Wizara imejipangia maalum kabisa! Kwamba, sisi mwaka wa fedha 2025/2027 tuwafikie vijana kadhaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nitoe pendekezo na ushauri; lazima kuwe kuna mwongozo maalumu wa kifedha, na kitaalamu katika Wizara zote, ili kuwasaidia wale vijana wajue kabisa kwamba, sisi katika Wizara yetu ya Madini tuna asilimia zetu ngapi? Pia, itakusaidia wewe, ambaye una-*supervise* tu katika zile Wizara za Kisekta kujua kwamba, mwaka huu Wizara ya Afya au Wizara ya Madini wamesaidiwa vijana wangapi? Wameweza kusaidia vijana wangapi? Wamefanikiwa wangapi, na hawajafanikiwa wangapi, ili hata unapofika mwaka wa fedha tunakuja kupima, hawa wamefanikiwa kwa nini, na hawa hawajafanikiwa kwa nini? Wanahitaji nini, ili waweze kusonga mbele? Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Latifa Juwakali kwa kufuatilia sana masuala ya vijana, na kwa kweli anawawakilisha vyema kabisa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la kwanza Serikali tumekuwa na utaratibu kila wakati kurejea na kufanya tathmini ya matokeo ya programu mbalimbali ambazo zinafanyika. Ninapenda tu kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba, kutokana na tathmini hii, baada ya kutathmini Sera ya Vijana ya mwaka 2007, ndiyo tukaja na Sheria ya mwaka 2019, Sura 290 ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ambazo zilisababisha kutengwa kwa 10%, kwa ajili ya makundi maalum, likiwepo kundi la vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hiyo ya sera iliyopita ndiyo ilisababisha kuja na Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura ya 410, ambayo pia, imegusa masuala ya kutenga fedha, kwa ajili ya makundi maalum. Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwamba, mwaka 2024 kanuni za utoaji mikopo zilirejewa, na ukiangalia kwa mfano, Serikali za Mitaa tumeongeza umri kutoka miaka 35 mpaka miaka 45 kwa vijana, ili kuongeza wigo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala la kuleta sheria kuhusiana na sekta maalum za ki-Wizara tutalifanyia tathmini, tutaangalia namna tunavyoendelea, na tunaendelea kupokea maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili la kuhusiana na kuwa na mwongozo maalum wa ki-Wizara; tunalipokea kama ushauri alivyoutoa. Kwa sasahivi, kupitia programu ya shilingi bilioni 200 ya uwezeshaji wa vijana pamoja na wanawake, tuna mwongozo maalum wa uwezeshaji vijana ambao tumeugawa katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru, ilikuwa ni moja ya mapendekezo yake kwamba, tuwe na maafisa viungo vijana katika Wizara. Napenda pia, kumweleza kwamba, tumelifanyia kazi, na Wizara zote 26 sasahivi zina maafisa viungo vijana, ambao wamepewa mwongozo, na wao ndio wanatupatia uratibu wa shughuli za vijana katika zile Wizara. Kwa hiyo, katika hilo tunachukua na tutaendelea kuliboresha katika utendaji wetu. Nninashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 52

Kuchochea Mapinduzi ya Kidijitali katika Shughuli za Kiuchumi na Kijamii

MHE. ESTHER E. MALLEKO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuchochea mapinduzi ya kidijiti katika shughuli za kiuchumi na kijamii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijiti wa Tanzania wa mwaka 2024–2034 *(Tanzania Digital Economy Strategic Framework 2024–2034)* unaoweka mwelekeo wa maendeleo ya uchumi wa kidijiti hapa nchini. Utekelezaji wa mkakati huu unalenga kuongeza mchango wa uchumi wa kidijiti katika Pato la Taifa, kuimarisha tija, na ufanisi katika shughuli za kiuchumi na kijamii, kupanua fursa za ajira na biashara, kuchochea ubunifu na uwekezaji, pamoja na kuboresha ubora na upatikanaji wa huduma za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi ni sehemu muhimu ya jitihada za Serikali za kujenga jamii ya kidijiti, na zinaunga mkono utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, swali la nyongeza!

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, katika kuelekea katika kujenga uchumi au jamii ya kidijiti kuelekea Dira 2050, nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha vijiji vyote, hususan katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro, vinapata mawasiliano mazuri na huduma ya *internet,* ili wananchi wetu waweze kufaidika na fursa hizi za kidijiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kama tunavyojua, huduma za *internet* zina gharama kubwa sana, na sisi tunatamani wananchi wetu, hasa wa vijijini, waweze kupata huduma hizi stahiki. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inapunguza gharama kubwa za *internet?*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza!

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Esther Malleko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza la mkakati wa Serikali; ni kwamba, Wizara ina mkakati wa miaka mitano wa ujenzi wa minara katika maeneo yote ya nchi hii, hususan maeneo ambayo yana changamoto kubwa ya mawasiliano. Kwa hiyo, ninapenda nikuhakikishie Mheshimiwa Esther, pamoja na Wabunge wote wa Bunge hili kwamba, ndani ya miaka mitano hii Serikali ina mkakati wa miaka mitano wa kujenga minara katika maeneo yote yenye changamoto ya mawasiliano nchini. Tuna hakika kwamba, ufikapo mwaka 2030 tutakuwa tumeimaliza changamoto hii kwa kiasi kikubwa, kama siyo kuitokomeza kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, la gharama kubwa za *internet;* Serikali inaendelea kujadiliana na watoa huduma mbalimbali, ili kuhakikisha kwamba, suala hili tunalifanyia

kazi kwa kufanya tathmini kuhusu gharama za *internet*. Yamekuwa ni malalamiko ya muda mrefu ya Waheshimiwa Wabunge na sisi, kama Wizara, tumekuwa tunashauriana na *TCRA*, na watoa huduma mbalimbali, na bado eneo hili tunalifanyia mashauriano. Ninaamini ndani ya muda mfupi tutalipatia ufumbuzi. Ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Ninamwita Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 53

Ujenzi wa Barabara ya Mtama – Newala

MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Mtama hadi Newala itajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba kwa ruhusa yako, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, niweze kutoa pole nyingi sana kwa Wananchi wa Jimbo langu la Ileje, ambapo kuna janga kubwa la moto ambalo linateketeza miti kwa takribani kata kama nne; Kata ya Ibaba, Kata ya Lubanda, Kata ya Kalembo, na sehemu ya Kata ya Ngulilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa tu taarifa Wananchi wa Ileje kwamba, Serikali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, na Wilaya ya Ileje, kwa ujumla wanalifuatilia sana tukio hili. Mimi mwenyewe nilienda huko kuwapa pole na kuona majanga ambayo yametokea, ambapo

nyumba zimeungua, lakini pia, kuna wananchi ambao wameathirika kwa hiyo, tunatoa pole nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mtama – Mkwiti hadi Newala, yenye urefu wa kilometa 74, kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea na ziko katika hatua za mwisho. Baada ya kukamilika kwa hatua hii Serikali itatenga bajeti, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, swali la nyongeza!

MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa majibu mazuri kutoka Serikalini, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri aliliambia Bunge lako Tukufu katika kikao cha mwezi wa kwanza, tulivyouliza swali lingine la nyongeza kuwa, katika barabara hiyo iliyotajwa, katika vipande vya lami, katika Vijiji vya Maputi, Kitangari, Mmovo na Amkeni vitawekewa taa za barabarani. Mpaka leo hakuna hata taa moja iliyowekwa! Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kuweka taa za barabarani katika maeneo hayo tuliyoyataja?

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili. Barabara hiyo ya Mkwiti – Kitangari mpaka Newala, ni ile barabara inayounganisha kutoka Dar es Salaam – Lindi, mpaka Masasi. Barabara ya Dar es Salaam mpaka Lindi ni mbovu, na katika barabara ile kuna mashimo mengi ambayo kwa hakika sijawahi kuona katika barabara zote katika nchi hii, zaidi ya Barabara ya Mtwara – Lindi mpaka Dar es Salaam!

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wametwambia, kama Serikali imeshindwa kuziba mashimo, basi kwangueni kile kipande cha lami, ili tuweze kupita kwenye vumbi. Je, ni lini sasa Serikali itakwangua hiyo Barabara, ili sasa tukubali tu hakuna lami, tupite kwenye barabara ya vumbi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nampongeza sana Mheshimiwa Nawanda kwa kuwasemea Wananchi wa Jimbo lake la Newala Vijijini, lakini pia, Wananchi wote wa Kusini, na Watanzania wote ambao wanatumia hiyo Barabara ya Dar es Salaam – Mtwara kwenda Masasi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na jibu la kwanza. Ni kweli tuliahidi kwamba, tutaweka taa za barabarani maeneo manne, ambayo tumeweka lami; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunavyoongea sasahivi tumepata mkandarasi, na ameagiza taa kuweka maeneo ya hivyo Vijiji vya Maputi, Kitangari, Mtangalanga, na baadaye Amkeni. Maeneo haya yatakwenda kuwekwa taa ambazo tayari zimeagizwa tunavyoongea sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya kutoka Dar es Salaam – Lindi hadi Mtwara; tunakiri, na tumekuwa tunasema. Tumewasikia Wabunge wengi kwamba, ni kati ya barabara ambazo zimeathirika sana kwa sasa. Kwamba, zina mashimo mengi na zimechoka!

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mipango miwili; moja, ni kuifanyia matengenezo barabara yote kwa kupata fedha, lakini kwa sasa tumeainisha maeneo ambayo kwa kweli, yamechoka sana, ambapo tumetenga fedha, na tutaanza kuzikarabati, siyo kutoa na kuacha vumbi, Hapana! Tutaanza kuzikarabati takribani kilometa 50 maeneo ambayo tumeyaainisha yameharibika sana, ili tuanze kwa awamu wakati tunatafuta fedha ya kukarabati wa barabara yote. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza!

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri kuwapa pole Wananchi wenzetu wa Jimbo la Ileje kwa janga la moto, poleni sana:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaosafiri kutoka Mikoa ya Kusini, wanalazimika kusafiri kilometa zaidi ya 300 kutoka Kibiti kufika Morogoro Mjini, lakini kwa kutumia mchepuko wa kupita Kibiti, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bigwa, Kisaki mpaka Morogoro Mjini, wanatumia kilomita chini ya 160. Wananchi wa Morogoro Kusini sasa wanataka kujua, ni lini ujenzi wa Barabara ya Bigwa – Kisaki utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Bigwa – Kisaki, kimsingi tumepata mkandarasi, amepata sehemu ya malipo ya awali, na alimeanza kujenga hata kambi ya ukandarasi. Sasahivi ambacho tunakiandaa, ni kumkamilishia malipo yote ya awali, ili aweze kuendelea na ujenzi wa hicho kipande ambacho amekabidhiwa.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Katani Katani, swali la nyongeza!

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu Barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara; ametoa majibu mazuri kwamba, watafanya ukarabati wa kuweka lami kilometa 50:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tunayoisema ina kilometa 600, na juzi ushahidi wa jambo hili, Mheshimiwa Waziri huyu wa vijana amepasua matairi mawili ya gari la Serikali. Hiyo tunasema gari ya Serikali, ambalo mnaweza kununua matairi, lakini Wananchi wa Kusini wanaitegemea barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotuambia kuna mpango wa kilometa 50! Tunaomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupe *commitment* ya ujenzi wa barabara ile! *Otherwise* mridhie sasa

kukwangua kabisa lami yenyewe tutembee kwenye vumbi, angalau magari yatapona! *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani katika Bunge tumeelezea, zile barabara ndefu, yaani zile shoroba za kiuchumi kubwa, ikiwepo na hiyo barabara. Hata hivyo, wakati tunatafuta hiyo fedha ya kutengeneza barabara yote, ambayo tunakubali kwamba, imechoka tumeainisha maeneo ambayo yamechoka zaidi kuliko maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara haichoki yote *uniformly*, kuna maeneo ambayo yalikuwa yamechoka sana. Yale ndiyo tumesema tumeyaainisha, ambayo hayatakuwa ni moja kwa moja kuitengeneza barabara moja kwa sasa, lakini yale maeneo ambayo tuna uhakika yamechoka sana, ndiyo tumeya-*spot*. Kwamba, hapa tutatengeneza pengine kilometa tano, pale ngapi, kufikisha hizo 50 wakati tunatafuta fedha yote ya kui-*rehabilitate* hiyo barabara kwa ujumla wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, swali la nyongeza!

MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nikiri wazi Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya ni miongoni mwa *encyclopedia* za Wizara ya Ujenzi. Kule kwetu Kisarawe, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu, Mwaka 2024 kipande cha barabara ya Kilometa 34.5, barabara ile inayotoka Kisarawe mpaka Mwanalumango kilitangazwa, na Disemba mwaka jana Wizara ilipata mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu, mwezi wa nne, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alikuja Kisarawe, na alitoa wiki mbili mkandarasi atapatikana kuweza kufanya ujenzi. Mwezi wa tano nikauliza swali; lini mkandarasi atafika, lakini nikajibiwa kwamba, si muda mrefu mkandarasi ataingia. Sasa ninaomba kujua, Je, lini mkandarasi wa Barabara ya Kisarawe – Mwanalumango, kilometa 34, ataanza kazi katika eneo lile?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kazi kubwa anayowafanyia Wananchi wa Kisarawe. Ni kweli kwamba, hiyo barabara tumepata mkandarasi, lakini ndiyo zile barabara nyingi ambazo zilikuwa zimesimama, ili kufanya miradi mingine, na kwamba, sasa ndiyo tumeanza kuwalipa wakandarasi zile fedha za awali, kwa maana ya *advance payment,* ili waweze kurudi barabarani, ambapo ni pamoja na hiyo barabara ya Mheshimiwa Jafo, kwamba itakuwa ni zile barabara ambazo ndiyo sasahivi kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopata hela, tunapeleka kuwapa wakandarasi, ili waweze kurudi *site* na kuanza kufanya kazi. Pia, tumekubaliana zile barabara ambazo zilikuwa zimesimama, ndiyo tutaanzanazo sasa, na ziko barabara ambazo tayari wakandarasi wameanza kupata fedha, na wanarudi *site* kufanya kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza!

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Serikali imefanya usanifu wa barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu, na wakati wa uzinduzi wa Daraja la Magara, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Philip Mpango, alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kilometa 48. Je, ni lini Serikali itaanza sasa kufanya utekelezaji wa matengenezo ya lami katika barabara hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara hiyo inaanzia Jimbo la Babati Vijijini, kwa Mheshimiwa Naibu Spika, kwenda kwa Mheshimiwa Mbunge. Tunaomba majibu! *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini. Bahati nzuri wakati Mheshimiwa Makamu wa Rais Mstaafu anatoa

ahadi kufungua Daraja la Magara, mimi nilikuwepo; ni kweli hiyo barabara ni muhimu sana, inatakiwa ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekamilisha usanifu, lakini kitu ambacho tumekifanya, ama tunaendelea kukifanya ni, kwanza wakati tunatafuta fedha kujenga barabara yote, kule kwenye *escapement*, kwenye ile miinuko mikali, tumeendelea kujenga kwa kiwango cha zege, ili walau magari yaweze kupit, huku tukiwa tunatafuta fedha ya kujenga barabara yote, kama ambavyo ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, ambayo ni maelekezo. Serikali inayafanyia kazi kuijenga barabara yote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Barabara ya kutoka Tarime – Mogabiri – Nyamongo – Mugumu – Serengeti, kinachofanyika kule ni aibu! Ni kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Tandahimba kwamba, wangekubali tu badala ya kuchukua udongo wanashindilia barabarani pale tunatukanwa, ile barabara waingekwangua ikabaki na vumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wamepata fedha zile ambazo wameanza kupeleka! Mkandarasi hayupo *site*, watu wanapata shida, watu wanapata ajali, tunapata misiba! Lini barabara hii itaanza kukamilishwa kuanzia Tarime Mjini – Mogabiri, Nyamwaga – Nyamongo, Nyamongo – Mugumu – Serengeti?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Tarime kwa kazi kubwa anayofanya na hasa kufuatilia hizi barabara. Hii barabara yenye vipande vitatu kutoka Tarime, pale Tarime Mjini; kutoka Tarime – Mogabiri, Mogabiri – Nyamongo hadi Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii iko kwenye *phase* tofautitofauti. Kilichokuwa kimetukwamisha ilikuwa ni malipo ya awali kwa wakandarasi, na hasa kutoka Nyamongo kwenda Serengeti; huyu wa hapa Mogabiri kwenda Nyamongo, ambaye alikuwa ame-*raise certificate*, zilikuwa hazijalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba, hizi barabara ninadhani jibu litakuwa ni lilelile. Kwamba, hizi barabara ndiyo zile ambazo kwa kweli, zilikuwa zinasuasua kwa sababu, zilikuwa zinasubiri malipo, kama siyo ya awali, basi ni yale ambayo tulikuwa tumepokea hati ya madai ya wakandarasi, ambayo Serikali imekuwa kwa kweli, inaandaa hayo malipo tunayopata, na kuwalipa, na kuwarudisha *site,* ambapo wengi walikuwa wameondoka maeneo ya kazi. Kwa hiyo, sasahivi tumewajulisha wakandarasi wote kuleta vifaa *site*, lakini pia, kuleta wataalamu, ili waweze kuanza kazi mara moja baada ya kuwa tumewalipa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Enock Zadock koola, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 54

Mgogoro wa Shamba la Lokolova - Vunjo

MHE. ENOCK Z. KOOLA aliuliza:-

Je, nini Kauli ya Serikali juu ya mgogoro wa Shamba la Lokolova lenye ekari 2,610?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Enock Zadock Koola, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la Chama cha Ushirika LOKOLOVA linafahamika kama Shamba Na. 70, lililopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. Shamba hili lililopangwa kwa matumizi ya kilimo na ufugaji, lina ukubwa wa ekari 2,610 na lilipimwa na kumilikishwa kwa Chama cha Ushirika cha *Ufugaji na Uzalishaji Mali Limited* (LOKOLOVA), kupitia Hatimiliki Na. 3619, kwa muda wa miaka 99, kuanzia tarehe 01 Julai, 1986.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro katika shamba hili unatokana na madai ya Wanakijiji wa Lotima na Makuyuni kutoshirikishwa wakati wa umilikishwaji wa ardhi hiyo kwa Chama cha Ushirika cha *Ufugaji na Uzalishaji Mali Limited* (LOKOLOVA), Mwaka 1986. Kutokana na hali hiyo, Chama cha Ushirika kilifungua Shauri la Ardhi Na. 577, la Mwaka 2024, dhidi ya wananchi hao katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Moshi, ambapo baada ya kusikiliza shauri hilo iliamriwa kuwa, Chama cha Ushirika LOKOLOVA ndiyo wamiliki halali wa shamba hilo, na wananchi waliopo ndani ya shamba wanapaswa kuondolewa. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Enock Zadock Koola, swali la nyongeza!

MHE. ENOCK Z. KOOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Nimepokea majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ni majibu mepesi sana:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuuliza maswali mawili. La kwanza; kuna ekari 140 ambazo Mwaka 2015, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliagiza yaweze kukabidhiwa kwa Halmashauri ya Moshi, ili na sisi tuweze kupata soko letu la kimataifa. Tumefuatilia kwa Mrajisi wa

Vyama vya Ushirika, na kwamba, wao wametoa idhini! Sasa ni lini hizo ekari 140 zitapewa Halmashauri ya Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; mwezi wa pili mwaka huu, tulikuwa na ugeni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, na alitoa maagizo na maelekezo kwamba, Ofisi ya TAMISEMI, kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, na Ofisi ya Wizara ya Ardhi, kuweza kukutana na hizi pande mbili, ili kuweza kubaini na kupata njia sahihi kutoa mvutano kwa huu mgogoro, ili waweze kukabidhiwa, tujue namna inaendelea, lakini mpaka leo miezi nane imepita bado hicho hakijafanyika. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari baada ya Bunge hili kuongoza hiyo *delegation*, wakishirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, kukaa na hizo pande mbili, ili sasa tupate jibu na suluhu ya mwisho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naendelea kumpongeza Mheshimiwa Enock kwa kuwa mfuatiliaji mzuri sana wa jambo hili, na mapenzi makubwa anayoonesha kwa wananchi wake. Ni kweli, jambo hili lina maslahi mapana kwa wananchi wanaolizunguka shamba hili, hususan vijiji hivyo viwili, ambavyo amevieleza, ninakushukuru sana:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza. Kama swali lake la nyongeza juu ya ekari 140; ninaomba nitumie nafasi hii kuliambia Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge asikie, kazi hii ya kumega ekari 140 imekamilika na taarifa yake imewasilishwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ambapo muda wowote ule basi, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itakuwa tayari kuwapa Halmashauri ya Moshi katika ratiba ambayo ataipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Ni kweli, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo hayo, na sisi pamoja na ofisi yake, chini ya TAMISEMI, tumekaa na kukubaliana, na Mheshimiwa Mbunge tutakushirikisha twende kwa pamoja na Ofisi ya Mkoa na Mkuu wa Wilaya, kwa ajili ya kwenda kutekeleza mazungumzo ya

pande hizo mbili, kadiri ya maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la Mheshimiwa Mbunge.

Tuendelee, Wizara ya Nishati. Swali la Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Mwera, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ali Khalil Mirza.

Na. 55

Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere

MHE. ALI KHALIL MIRZA K.n.y. MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere?

NAIBU SPIKA: *(Hasikiki)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Jimbo la Mwera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere umekamilika kwa asilimia 100, tangu tarehe 23 Februari, 2025 na kuzinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 22 Agosti, 2026. Kwa sasa mitambo yote inafua umeme wenye jumla ya Megawati 2,115 ambazo zinaingizwa kwenye Gridi ya Taifa kutokana na mahitaji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa pongezi kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi lilivyoshiriki kusimamia mradi huu hadi kukamilika. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mbunge, una maswali ya nyongeza? Hakuna.

MHE. ALI KHALIL MIRZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunashukuru sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Wizara ya Madini. Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Kahama Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 56

Mkakati wa Serikali Kusimamia Wamiliki wa Leseni za Uchimbaji Madini

MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusimamia wamiliki wa leseni za uchimbaji madini ya dhahabu, ili kuleta nafuu kwa wachimbaji wadogo?

NAIBU SPIKA: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Kahama Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasimamia wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini kwa kuzingatia Sheria ya Madini, Sura ya 123, hususan Kanuni za Haki Madini za Mwaka 2018; Kanuni za Madini kuhusu Ulinzi wa Mazingira kwa Wachimbaji Wadogo za Mwaka 2010, kupitia usimamizi wa Mpango wa Ulinzi wa Mazingira *(Environment Protection Plan – EPP),* pamoja na

Kanuni za Madini kuhusu Usalama, Afya Kazini, na Ulinzi wa Mazingira za Mwaka 2010. Sheria na kanuni hizo zinawataka wamiliki wa leseni kutekeleza masharti ya leseni zao kwa kuzingatia usalama, afya, na utunzaji wa mazingira katika shughuli za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Tume ya Madini, na Ofisi za Maafisa Madini Wakazi, walioko kila mkoa, Serikali inaendelea kuimarisha ukaguzi wa migodi, usimamizi wa shughuli za uchimbaji, utoaji wa elimu, na msaada wa kitaalamu kwa wachimbaji wadogo, utatuzi wa migogoro, na uchukuaji wa hatua za kisheria dhidi ya wanaokiuka sheria na masharti ya leseni. Hatua hizi zinalenga kuongeza tija na usalama katika shughuli za uchimbaji, kuimarisha utunzaji wa mazingira, kulinda haki, na maslahi ya wachimbaji na wawekezaji, na kuhakikisha rasilimali za madini zinaendelezwa kwa kuzingatia sheria kwa manufaa endelevu ya wananchi, na Taifa kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, swali la nyongeza!

MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja. Wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wamekuwa wakichora maduara yao kwenye maeneo ya wenye leseni. Watu wenye leseni hawa wamekuwa wanaweka tozo mbalimbali, ikiwemo kuweka mirabaha kwa mawe yanayochimbwa kwenye maduara hayo, na tozo zingine mbalimbali ambazo zimekuwa ni tozo holela! Je, Serikali kupitia Wizara yetu ya Madini, haioni sasa umuhimu wa kuweka miongozo, sheria, na kanuni zinazodhibiti tozo na mirabaha holela, ili kuwalinda wachimbaji wetu wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha upimaji wa leseni ambazo zinamilikiwa na Serikali, ili kuwapatia wachimbaji wadogo wasiokuwa na leseni,

kuweza kuwekeza, na kuchimba katika maeneo hayo, na kukuza kipato chao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Ngayiwa kwa jinsi ambavyo ameleta hoja za msingi katika haya maswali mawili ya nyongeza; la utetezi wa wachimbaji wadogo, na hasa wale ambao hawana leseni:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande huu uchimbaji unaofanyika kwenye maduara, Kanuni ya 5A, na kipengele kidogo cha kwanza cha Kanuni za Haki za Madini, ambayo imerekebishwa Mwaka 2025, inawataka wamiliki wa leseni wawe wanaandaa mikataba na hao wachimbaji wa maduara, na mikataba hiyo kuletwa Tume ya Madini, kwa ajili ya kusajiliwa, na kwa njia hiyo Tume ya Madini iweze kuwadhibiti. Kwanza, dhidi ya ugawaji wa mawe kwamba, wanayagawa kwa uwiano wa ile mikataba yao. Pili, kwa ajili ya kusimamia kuepusha uwezekano wa kutozwa tozo za kiholela anazosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipengele cha mirabaha; ninaomba ilieleweke kwamba, mirabaha yote katika sekta ya madini hukusanywa na Serikali, siyo wajibu wa wenye migodi, wala wenye miduara, na hukusanya kwa mujibu wa mamlaka iliyowekwa ya kutoza mrabaha wa kuanzia 1% mpaka 7%, pale ambapo madini husika yanaelekezwa na sheria. Ndiyo maana kwenye mirabaha yetu, haswa ile ya halmashauri 0.3%, hutozwa kupitia mfumo huo wa Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili; Serikali imechukua hatua madhubuti ya kufuta leseni mbalimbali ambazo haziendelezwi, na hatua inayoendelea sasahivi ni utafiti wa kina. Kwa wale ambao mmefuatilia kwenye vyombo, mmeona tumerusha ndege Kanda ya Ziwa, kwa ajili ya kubaini maeneo ya kuwagawia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulirusha pia, ndege nyingi katika maeneo ya Bassoutu, kwa ajili ya kubaini maeneo mapya ya

kupata madini. Pia kuna mikakati madhubuti ya Serikali, kupitia uwekezaji mkubwa wa kutumia kampuni za kigeni, kufanya utafiti wa kina, ili kubaini maeneo ambayo yana uwepo wa madini, na wachimbaji wadogo ambao bado hawana leseni waweze kupata leseni za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali kupitia *GST* inaendelea kupanua wigo wa maeneo yenye uwepo wa madini yaliyobainishwa kutoka 16% ya sasa hadi kufikia 50% ifikapo Mwaka 2030. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Haidary Sumry, swali la nyongeza!

MHE. HAIDARY H. SUMRY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, madini ya dhahabu tayari yanakuwa ni pesa kwa sababu, thamani yake inajulikana kwenye soko. Wachimbaji wamekuwa wanapata changamoto kubwa sana kwa kushindwa kuifanya dhahabu kama dhamana, kwa maana ya kwamba, ana dhahabu yake, labda kilo tano, hataki kuiuza sasa, lakini anataka pesa labda 50% ya ile dhahabu kilo tano, ili aweze kuendelea na shughuli zake za uchimbaji kwenye mgodi wake, na amekuwa anashindwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima aiuze hiyo dhahabu, ili aweze kupata pesa aweze kuendelea na shughuli. Sasa, ni lini Serikali itatambua dhahabu kama dhamana, ambayo mchimbaji anaweza akaiweka benki na akapewa pesa, labda 70% ya bei ya soko iliyopo, ili akaendelee; na ile dhahabu ikabaki kama dhamana, halafu pindi atakapoamua kuiuza atauza na kurudisha ile pesa aliyoichukua, ili kuweza kuwasaidia wachimbaji wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; sasahivi bei ya dhahabu imeshuka kwa hiyo, inamlazimisha mchimbaji kuuza

kulingana na bei ya soko la sasahivi, lakini inawezekana kwa majira ambayo yanajulikana, kuna kipindi maalumu ambacho dhahabu huwa inapanda bei, na kuna kipindi dhahabu huwa inashuka. Ninaomba majibu ya Serikali, ili kuwasaidia hao wachimbaji wadogo, na wachimbaji wa Kitanzania, ambao wanafanya kazi kwenye eneo hilo? Ninaomba kuuliza swali hilo la nyongeza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa swali zuri la Mheshimiwa. Ninaomba tu ieleweke kwamba, madini ya dhahabu, kwanza kwa sasahivi, na kwa sababu, nchi yetu imeruhusu wawekezaji mbalimbali kujenga *refinery* za kusafishia dhahabu, mpaka ipatikane dhahabu safi yenye ubora wa 99.99%; mchimbaji yeyote mdogo, ambaye anaweza akasafisha dhahabu yake ikawa safi anaweza, na anaruhusiwa, kwenda kuhifadhi kwenye Benki Kuu, kama akiba yake ya kifedha ya thamani ya yale madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kuweza kuweka kama dhamana, kwa ajili ya kukopea kwa kuendeleza uchimbaji, au kuweka madini mpaka thamani itakapopanda tena zaidi, hilo ni suala ambalo Serikali imelisikia, na taratibu za kufanya hivyo. Tunalipokea, kama ushauri ambao tunaweza tukafanyia kazi. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu mazuri kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Ninamwita Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 57

Ujenzi wa Mabwawa ya Umwagiliaji, Vwawa

MHE. JAPHET N. HASUNGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga mabwawa ya umwagiliaji katika Kata za Iyula, Mlangali na Itezya, ili kuboresha zao la kahawa katika kata hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza kilimo cha zao la kahawa nchini, Serikali kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania na wadau wa maendeleo, inaendelea kutekeleza mpango wa kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbalimbali za kilimo, ikiwemo kilimo cha umwagiliaji katika zao la kahawa. Lengo ni kuongeza tija na uzalishaji, pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kupitia mpango huo, jumla ya visima virefu 20 vimechimbwa Wilayani Mbozi katika vijiji vya Iwezi, Isansa, Naulongo, Iporoto, Isela, Hampangala, Wasa, Ichesa, Ibembwa, Mbozi, Itepula, Insani, Bara, Sambwewe, Shaji, Igale, Ihowa, Nambinzo katika Jimbo la Mbozi, Lumbila pamoja na Idunda katika Jimbo la Vwawa, ambapo takribani wananchi 7,900 wananufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa visima hivi unahusisha uwekaji wa miundombinu zikiwemo pampu, mitambo ya sola, na matanki ya kuhifadhia maji. Vilevile katika mwaka wa fedha 2025/2026, wadau wa maendeleo katika tasnia ya kahawa, Shirika Lisilo la Kiserikali la *Good Neighbours* limekamilisha ujenzi wa bwawa katika Kata ya Itumpi, ambalo limekabidhiwa kwa wakulima wa zao la kahawa, ili kuwawezesha katika kuboresha tija ya zao kupitia kilimo cha umwagiliaji. Pia, Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi inaendelea na utambuzi wa maeneo yenye wakulima wengi wa kahawa, kwa ajili ya kuendelea na mpango wa uchimbaji wa visima.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, swali la nyongeza!

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, na ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa, japo majibu yenyewe yanachanganya vijiji vilivyopo kwenye Jimbo la Mbozi na Jimbo la Vwawa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za mezani zinaweza zisiwe na uhalisia zaidi kuliko ukienda *field*. Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa tayari baada ya *session* hii kumalizika, kuambatana na mimi, ili twende tukaone ni vijiji vipi vimenufaika na hivyo visima katika Jimbo la Vwawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, swali la msingi lilikuwa linauliza ujenzi wa mabwawa katika Kata ya Iyula, Mlangali na Itezya, na ndivyo lilivyokuwa linataka, lakini majibu yameenda tofauti kidogo! Sasa ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, tunachimba mabwawa kwenye hayo maeneo niliyoyataja?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, kisima kimoja kwenye kijiji hakiwezi kukidhi mahitaji ya umwagiliaji, lakini bwawa linaweza likatumika na wananchi wengi zaidi wakapata huduma hiyo, na mashamba yanaweza kupanuka. Sasa upi mkakati hasa wa kuhakikisha mabwawa yanaanza kujengwa katika kata hizo nilizozisema? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kaka yangu, Mheshimiwa Hasunga. Namthibitishia tu moja kwamba, tutafanya ziara pamoja, na tutapita katika maeneo yote ya Jimbo lako la Vwawa, na utakuwa ni ule wakati ambao ninaelekea Tunduma, kwa hiyo tutafanya pamoja hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninamthibitishia tu kwamba, tuna mikakati ya aina mbili; kuna mikakati ambayo inatekelezwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, halafu tuna mikakati ile ambayo

inatekelezwa na Bodi ya Kahawa katika kuwawezesha wakulima. Hata hivyo, kwa asilimia kubwa watu wa Bodi ya Kahawa wamejikita katika uchimbaji wa visima, na ndiyo maana wana magari yale, kwa ajili ya kuchimbia visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo utaona sasahivi wanaenda katika maeneo yote, hata kule Ruvuma wanakolima kahawa, Kagera, pamoja na Mbozi huku, maeneo ya kwetu, kwa ajili ya kuwasaidia wale wakulima kwenye eneo dogo la watu kadhaa; tunawachimbia, tunawawekea pampu na mifumo, ili kuweza kuwasaidia. Kwa hiyo, katika ile mikakati ya tume tutahakikisha haya maeneo tunayapelekea hii miradi, ambayo Mheshimiwa Mbunge umekuwa ukiiainisha, ili sasa isaidie kahawa, pamoja na mazao mengine ambayo wakulima watakuwa wanatumia. Kwa hiyo, hilo ninakuthibitishia, na nitalisimamia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza!

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninaishukuru sana Serikali kwa kutujengea Bwawa la Kilanya; ninajua wako kwenye hatua za mwisho za kumalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninauliza swali kwa Serikali; Serikali imefanya *feasibility study* kwenye Bwawa la Borutu, Natron, Makeresho, Kikafu Chini, pamoja na Kimashuku, lakini mpaka sasahivi ujenzi haujaanza. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga mabwawa haya, ambayo ni muhimu sana kwa Wilaya ya Hai?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninampongeza kwa maswali ya msingi, Mheshimiwa Dkt. Saashisha Mafuwe, na kwa kweli, umeyauliza kidokta zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namthibitishia tu kwamba, nimezungumza na Mkurugenzi wa Umwagiliaji, kaka yangu Raymond, na amenithibitishia tu kwamba, maeneo haya

feasibility study imekamilika kwa hiyo, sasahivi anachosubiri ni fedha tu ambazo tukipokea, maana yake tutapeleka wakandarasi *site*. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *status* ambayo tukonayo sasahivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukipokea fedha, maana yake sasa tutakwenda katika hatua ya kukabidhi wakandarasi *site,* ili waanze ujenzi. Kwa hiyo, waambie wananchi wa Hai kwamba, Serikali ipo kazini na inakuja, kwa ajili ya utekelezaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum. Ninamwita Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Katavi, sasa aulize swali lake!

Na. 58

Hatua kwa Wanaosapoti Vitendo vya Ushoga

MHE. THOMAS K. MAGANGA aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa akinamama wanaoonekana kwenye matukio ya sherehe, kuunga mkono vitendo vya kishoga Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imezindua Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili wa mwaka 2026/2027–2036/2037. Mkakati huu unalenga kuimarisha elimu kwa umma na uratibu wa wadau wa kisekta, ikiwemo sekta binafsi, na jamii kukabiliana na vitendo vinavyochangia mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya sherehe za kijamii huombewa kibali cha Afisa Utamaduni, kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, lengo likiwa ni kudhibiti sherehe hizo kukidhi staha na maadili ya Kitanzania. Hivyo, ninatoa wito kwa Watanzania kutoa taarifa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Polisi pale wanapowabaini wanaokiuka maadili, miiko, na tamaduni za Kitanzania kwa hatua stahiki, kuanzia kwa walioandaa sherehe, waongoza sherehe, pia wanawake au wanaume wanaoshabikia mambo kinyume na maadili, miiko, na tamaduni za Kitanzania kwenye sherehe hizo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, swali la nyongeza!

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninaipongeza sana Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Vikundi Maalum, kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi. Wanafanyakazi nzuri sana:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi, tunatambua Serikali inao utaratibu na mpango ambao umeuongea, Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kwa sasa hali ni mbaya! Serikali ina mpango na mkakati gani wa kudhibiti hii hali, wakati tunasubiri ule mpango uanze kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Matukio mengi sana yanayofanyika Dar es Salaam kwenye hizi shughuli za ngoma, yanashabikiwa sana na akinamama! Je, Wizara ina mpango gani wa kuishirikisha Wizara ya TAMISEMI, ili Wenyeviti na Watendaji wa Kata waweze kushughulikia mambo haya, ili mambo ya mmomonyoko wa maadili na ushoga yasikue kwa kasi kwenye mitaa yetu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Kampala kwa kazi kubwa anayoifanya; ni Balozi wa Wizara yetu katika kitengo

hiki, na amekuwa mzalendo. Anaifanya kazi hii kwa bidi na uzalendo mkubwa, bila kujali kupata chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mkakati huu wa Taifa umeanza kazi. Hapa kikubwa ninachoweza kusisitiza ni ushirikiano, namna ambavyo Balozi Kampala anafanya kazi hii nzuri, nawasihi; sisi Wabunge wote, vilevile jamii kwa ujumla tuone kwamba, tunaendelea kusisitiza mila, desturi, na tamaduni salama ziendelee kuzingatiwa. Vilevile, kusisitiza hasa kwa kizazi hiki kipya kiendelee kujua kwa nini wazazi wao tumeweza kufika hatua hizi za kuweza kuijenga nchi kwa sababu ya mila na desturi salama. Kwa hiyo, ninawaomba wote tuweze kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuzingatie kwamba, familia ndiyo msingi wa maadili ya kizazi. Kwa hiyo, wazazi wote, pamoja na majukumu makubwa tunayoendeleanayo ya kujitafutia mkate wa kila siku, tusisahau watoto wetu, tusisahau familia zetu; tuhakikishe tunatimiza wajibu wetu kikamilifu katika malezi na makuzi ya familia zetu. Tuongee na watoto wetu bila kuchoka mara kwa mara. Usiongeenaye leo ameenda chuoni, au anaenda shuleni, ukaona umemaliza! Ukipata nafasi unaongeanaye tena mara kwa mara, ili kuhakikisha watoto wanakuwa na maadili mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali, tutaendelea kushirikiana na Wizara zetu; Wizara ya wenzetu kwa sababu, hii ni Wizara mtambuka tunafanya kazi na TAMISEMI. Kama hapa umeona, tunafanya kazi na Wizara ya Utamaduni, Habari, Sanaa na Michezo, vilevile tunafanya kazi takribani na Wizara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuhakikisha Wenyeviti wa Mitaa, Watendaji wa Vijiji, na Kata, waweze kuwajibika ipasavyo. Vilevile, sisi tuna Maafisa Maendeleo kwenye kata zote nchini, ni kata chache sana ambazo hazina Maafisa Maendeleo. Kwa hiyo, na wenyewe pia, tutataka waweze kufanya majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakiweza kushirikiana kwa pamoja, tunaamini hawa vijana wetu ambao wanakengeuka

watarejea kwenye mstari, na itakapobidi kuchukua sheria au adhabu kali zaidi, tutafanya hivyo tukiamini kwamba, asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Kwa hiyo, tutafanya msisitizo kuona kwamba, wanatii mila na desturi salama.

NAIBU SPIKA: Ahsante. tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum! Litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Lucy Mwakyembe.

Na. 59

Mikakati ya Serikali Kuongeza Ajira Rasmi kwa Wanawake

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE K.n.y. MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuongeza ajira rasmi kwa wanawake, na kuongezea ushiriki wao kwenye uchumi jumuishi na ustawi wa jamii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika kuongeza ajira rasmi kwa wanawake, na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uchumi jumuishi na ustawi wa jamii, Serikali inafanya yafuatayo kwa uchache:-

(i) Ifikapo Mwaka 2050 angalau 50% ya Watanzania wawe na ajira zenye staha katika sekta rasmi, sambamba na kuongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi ambapo, hadi kufikia Juni, 2026 wanawake walio katika ajira rasmi kwenye sekta ya umma wamefikia 43%;

(ii) Kuongeza ushiriki wa wanawake katika mfumo wa ubunifu, ikiwemo kuanzisha vituo atamizi vinavyoweka kipaumbele kwa biashara na ubunifu unaoongozwa na wanawake. Pia, kuongeza biashara changa zinazomilikiwa na wanawake kwa 30% ifikapo Mwaka 2040;

(iii) Kuwawezesha wanawake kushiriki katika fursa za zabuni za 30% ya ununuzi wa umma kwa taasisi za umma, kutenga 30% ya ununuzi wa mwaka, kwa ajili ya makundi maalumu ambapo, kuanzia Mwaka 2023/2024 hadi Mwaka 2025/2026, jumla ya vikundi vya wanawake 394 vimepata tuzo 944 zenye thamani ya shilingi bilioni 23.34;

(iv) Kuwawezesha wanawake kutumia majukwaa ya kidijiti kama iSOKO yenye lengo la kukuza biashara za wanawake ambapo, kufikia Mwezi Juni, 2026 Jukwaa hilo limeweza kusajili jumla ya wanawake 24,269;

(v) Kuimarisha majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ambayo hadi kufikia Julai, 2026 yamefikia 15,147; na

(vi) Kutekeleza utaratibu wa mikopo ya 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri bila riba ambapo, wanawake ni asilimia nne.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Lucy Mwakyembe, swali la nyongeza.

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninapenda kuipongeza sana Serikali kupitia Wizara hii ya Wanawake na Jinsia ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Gwajima. Pia ninapenda sana kumpongeza ndugu yangu, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaona kuna mpango mzuri wa Serikali kuhakikisha 50% ya wanawake wanakuwa kwenye ajira za staha hadi kufikia Mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mkakati wa Wizara katika kuhakikisha mpaka kufikia Juni, 2026 imeweza kuajiri wanawake 43% kupitia sekta ya umma. Ninapenda kupongeza, kwa ajili ya mpango mzuri ambao umewekwa kupitia majukwaa ya kidijitali, kuweza kuwasajili wanawake 24,269 na ninapenda kuiomba Serikali iongeze kasi katika usajili wa wanawake hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Neema Majule; kutokana na majukumu ya kibaiolojia kwa wanawake, wanawake wengi wamekuwa wanakwama kupitia ajira hizi, lakini ninaomba kushauri au kuiuliza Serikali. Wana mkakati gani kutokana na wanawake hawa kuwa katika majukumu ya kibaiolojia, hususan kujifungua na kunyonyesha, ili kuwaajiri wengi katika kazi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Samahani, ninaomba arudie pale mwishoni, wawapo kwenye *maternity,* kufanyaje?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge.

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani katika kuongeza ushiriki wa wanawake hawa katika ajira wanapokuwa katika hali ya kujifungua au kunyonyesha wakiwapo kazini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninapende kumpongeza Mheshimiwa Lucy Mwakyembe kwa uwakilishi mzuri, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Neema Majule. Pia, ninakushukuru kwa pongezi kwa Serikali, kwa hakika Wizara tunajitahidi kuona kwamba, wanawake hawaachwi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu kuongeza kasi, kama ushauri wako; nimeupokea na ninaamini watendaji wetu wamesikia. Kasi itaongezeka kwa sababu, tuna malengo mazuri kabisa ya kuhakikisha kwamba, wanawake tunaendelea kwenda nao pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuhusu majukumu wakati wakiwa kwenye *maternity,* watawezaje kuendelea na kazi zao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi, kama Serikali, tumeendelea kusisitiza kila ofisi iwe na chumba maalumu, kwa ajili ya kunyonyeshea ama kukaa na mtoto yule, ambaye anahitaji huduma ya mama mzazi moja kwa moja. Kwa hiyo, tunaendelea kutoa wito, majengo yale mazuri ambayo leo Mheshimiwa Rais anayazindua Mji wa Serikali, Wizara zote zipo pale, ni makubwa kwa hiyo, Wizara zote; kwanza tuanzie kwenye *level* ya Wizara kuhakikisha tunakuwa na vyumba maalumu, kwa ajili ya hawa *lactating mothers,* au wote ambao wapo katika wakati wa kunyonyesha, ama malezi ya mtoto, yale ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ngazi ya mikoa wana nafasi pia, ya kuweza kuona kwamba, wanatenga vyumba katika majengo ya ofisi za wakuu wa mikoa, ili wale wafanyakazi wote walioko pale wanaopitia hatua ya kulea watoto wachanga, basi na wao waweze kupata nafasi ya staha ya kuhudumia mtoto wao katika mahitaji yale muhimu kabisa. Vilevile, katika ngazi zote tutaendelea kusisitiza, kulingana na miundombinu, basi tuwe na vyumba wezeshi, kwa ajili ya akinamama hawa waweze kuhudumia watoto na vile vile waendelee kutimiza majukumu yao.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwetu na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninawaletea matangazo.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza, tuna wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe ambao ni wanafunzi wenzao waliosoma pamoja katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino cha Jijini Mwanza, mwaka 2010. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Ndugu Evelyn Isaac Mfinanga, ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume; ambao ni viongozi wa CCM na wapigakura kutoka Jimbo la Morogoro Vijijini, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo:-

Tunaye Ndugu Mohamed Ausi na Bonaventura Benedict kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE),* Kampasi ya Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Timu ya wataalamu saba wa mafunzo ya biashara kutoka Dar es Salaam, Mwanza, na Zanzibar, wakiongozwa na kiongozi wao, Ndugu Baraka Nyorero. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waimbaji 14 wa kwaya ya *ABC* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao watoto nane wanaoishi mazingira magumu wa Shirika la *Compassion International Tanzania. (Makofi)*

Tunao wanafunzi 41 na walimu watano wa Shule ya Awali na Msingi ya *Peacock* ya Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 46 na walimu sita wa Shule ya Sekondari Mtakatifu Ursula ya Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Tunao wanachama 20 wa taasisi ya *Everlasting Kingdom Praise and Worship Ministry* ya Jijini Mbeya. Karibuni sana wageni wetu hapa Bungeni, Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028

na

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano; tutaanza na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda. Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima, ajiandae.

Ninaomba tuendelee na Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda!

MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Mpango wa Maendeleo ulioko mbele yetu wa mwaka 2027/2028. Awali ya yote na mimi ninaomba niwapongeze sana Wizara ya Mipango kwa wasilisho zuri ambalo amefanya Mheshimiwa Waziri, Prof. Kitila Mkumbo. Kwa kweli, ule ulikuwa siyo mpango tu, ule ni mkakati ambao ukiweza kutekelezwa vizuri utatutoa, na utaweza kufanikisha mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, ule mpango ukiusoma kwa ufasaha, kwa sura zote ambazo wamezieleza na kuzifafanua, unaona namna ambavyo wamefanya kazi kubwa. Pia, hata hao wenyewe, na Serikali inakiri kwamba, ili tuweze kufanikiwa vizuri hasa kwenye masuala ya uwekezaji wametambua mchango wa sekta binafsi wakiamini kwamba, ina uwezo mkubwa wa kuchangia zaidi ya 70% kwenye maendeleo ya nchi yetu na hata upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu kwa sababu, yapo mambo mengi, na wachangiaji wameeleza mambo mengi, ninaomba nijikite kwenye kuchangia mambo mawili mahsusi kwenye mpango huu wa maendeleo. Jambo la kwanza; ninaomba nichangie kuhusu ukuaji wa uchumi, ajira, na pato la mwananchi. Lingine ni usawa, mgawanyo wa rasilimali, na maendeleo ya mikoa na halmashauri zetu tukiamini kwamba, kwenye maeneo haya ushauri tutakaoutoa sisi Wabunge utaenda kusaidia kuweza kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba, utekelezaji mzuri wa mpango huu unahitaji fedha. Tutaongea mambo mengi sana hapa, lakini kama hatuna makusanyo ya kutosha, kama hatujaweka mikakati madhubuti ya kupata makusanyo ya kutosha, hatutaweza kutekeleza mpango huu. Utakuja huu wa 2027/2028, utakuja tena wa 2028/2029, mwisho hatimaye utakuja tena wa 2029/2030 wakati bado tunaongea yale yale!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, la kwanza; watusaidie watu wa Serikali kwamba, ili tuweze kufanikiwa ni lazima Serikali iweke mikakati inayopimika ya upatikanaji wa fedha na hatua za

kuchukua iwapo hatutaweza kufikia malengo tuliyoyatarajia kwenye mpango. Yaani, nini kitakuwa *fallback position* ya mpango huu iwapo yale ambayo tumeyapanga hakutakuwa na utekelezaji ambao unatakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, ukiangalia kwenye mpango mzima tumeona sehemu kubwa inayotegemewa ni sekta binafsi. Hata kwenye *PPP* wameeleza, hasa kwenye miradi ya uzalishaji kwamba, kwa miradi ya uzalishaji *PPP* haijafanya vizuri sana, ni kama 0.4 tu ya asilimia ya miradi, ambayo ilitegemewa ifanywe na *PPP,* lakini hakuna mtu ambaye anaweza kuja kuwekeza hapa, hasa kwenye viwanda vya uzalishaji kwa sababu, hatuna malighafi za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata leo wazalishaji wa ndani, wawekezaji wa ndani, tukichukulia tu ambao wamewekeza kwenye sekta ya kilimo; ukiangalia viwanda tulivyonavyo ni *primary industry* tu, ambavyo vinafanya kazi ya *ginnery,* na vyenyewe vinafanya kazi kwa miezi isiyopungua mitatu mpaka sita! Kwa hali hiyo utawezaje kuzalisha ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni ndani ya miezi mitatu, miezi sita, mwekezaji huyu amefunga kiwanda akisubiri tena msimu mwingine. Kwa hiyo, hatutaweza kuvutia uwekezaji, kama hatutakuwa na uwezo wa kuzalisha malighafi za kutosha kwa wawekezaji, kwanza wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia mpango huu, hauoni ile mikakati thabiti, ambayo itatuwezesha, kama nchi, kuwa na uzalishaji wenye tija. Ukiangalia kwenye mpango, hasa kwenye ukuaji wa ajira na uchumi na hasa wa mtu mmoja mmoja, tunazo programu na mifuko zaidi ya 75, ambayo mingine ipo chini ya Wizara ya Kilimo, mingine ipo Wizara ya Mifugo, mingine ipo Wizara ya Fedha, mingine ipo TAMISEMI!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mifuko na programu hizi, zipo fedha nyingi na sasa, mfuko wa juzijuzi ambao tumeupitisha, Mfuko wa Halmashauri wa 10%. Mifuko hii lengo lake lilikuwa ni kwenda kuongeza ajira pia, na kuongeza uzalishaji. Leo tukifanya

evaluation, tukifanya tathmini ya kina ya moja kwa moja ya mifuko hii na hizi programu; kwa mfano, ukichukua programu mbili ambazo zimefanya vizuri sana, ipo programu moja ya *MIVARF,* na pia, *ASDP I* na *II*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hizi zimefanya vizuri sana na zote zimefika mwisho. Hata leo ukifanya *evaluation* ya programu hizi, *MIVARF,* kwa watu waliotoka vijijini wanajua; *MIVARF* zilijenga *collection centers* za mazao, lakini leo mazao yanafuatwa shambani na wageni! Kwa mfano, leo ukienda Njombe, ndugu zetu wa Kenya, hatukatai wakulima wauze viazi na mazao mengine ya parachichi, mkulima anafuatwa shambani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata ile *bargaining power* haitakuwepo! Kwa hiyo, maana yake ni sisi bado ni wazalishaji wa *raw material* kwenda kwa wenzetu! Ndiyo maana hatuwezi kuvutia uwekezaji, hasa wa viwanda vya ndani ambavyo ndiyo vitazalisha ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua yapo maeneo ambayo Serikali imefanya vizuri sana. Kwa mfano, kwenye sekta ya madini; tuwapongeze na tuwapigie makofi Serikali, wamefanya vizuri kwenye programu ya kuwasimamia wachimbaji wadogo. Leo hii tunakiri kwamba, sekta ya madini ndiyo ambayo inachangia *export levy* kubwa nchini kuliko kitu kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sisi Tanzania wa kusubiri madini peke yake? Mbona tunazo rasilimali nyingi ambazo tunaweza kufanya *export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunazo *untapped revenue* nyingi kwenye sekta ya kilimo, ambazo tunaweza tukafanya *export* kwa mpango uleule uliotumika kwenye sekta ya madini kwa kusaidia wachimbaji wadogo. Leo heshima ya wachimbaji wadogo imeongezeka, sasa tunaona wengine wamekuwa ni wawekezaji wa ndani, na fedha zao zinazunguka kwenye ukuaji wa uchumi wetu na kwenye pato la mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo, na hasa Wizara ya Mifugo, tunazo *ranches* zipatazo 15 nchi hii. Zile ni *prime area* za *investment,* lakini ukiangalia *economic value* yake kwenye mchango wa Pato la Taifa, ambapo tukikusanya fedha hizi ndiyo tunakwenda kufanya uwekezaji, Waheshimiwa Wabunge hapa wengi wamelalamika kuhusu miradi ya maendeleo, hasa barabara, kwamba hazipitiki! Hatutaweza kujenga barabara hizi kwa kusubiria tu *PPP* peke yake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *private* sector wanaangalia kwenye miradi ambayo ita-*break even* mapema; mtu hawezi kuja kuweka fedha zake kwenye barabara ambazo hazina mzunguko wa kibiashara. Hata ingekuwa ni wewe huwezi kwenda kuwekeza fedha zako, ukajenga barabara ambapo mzunguko wa biashara ndani ya nchi hiyo hauwezi kukulipa mapema! Huwezi kupeleka fedha zako!

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ranches* hizi ni *prime area!* Hizi ni kama vitalu vya madini! Mkoa wa Kagera peke yake una *ranches* tisa! Ushauri wangu, hebu tuje na *revamping strategy* kwenye maeneo haya ya kiuchumi tuweze kuwekeza na kupata fedha; leo, hata ukiamua tu ukazipeleka *DSE* hizi *ranches,* utapata wawekezaji. Pia, tunao wawekezaji wa ndani ambao wanaweza kuwekeza kwenye *ranches* hizi tukapata malighafi, tukapata *products* za kusafirisha nje. Leo sisi kweli, kwa wingi wa mifugo tuliyonayo tunazidiwa na Namibia kusafirisha nyama nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Dodoma ukitafuta *beef steak* huwezi kuipata! Leo ukitafuta *sausage* za Tanzania, huwezi kuzipata, lakini ni kweli, tunao wawekezaji wa ndani wanaweza wakazitumia *ranches* hizi vizuri, kama ambavyo tumefanya vizuri kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wabadilishane *notes* hawa watu; mifugo na madini waone ambavyo sekta ya madini, mwanzo tulikuwa tunalalamikia sana Bungeni kwamba, haichangii vizuri, lakini sasahivi wamejipanga, wanachangia vizuri, na tumeona matajiri ambao wanatokana na sekta ya madini. Tunataka pia,

wawekezaji wa ndani watakaoendelea kutokana na sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizifanya sekta hizi vizuri hasa sekta ya mifugo kwa kutumia *ranch* zetu tutapunguza migogoro ambayo alikuwa anaeleza jana Mheshimiwa Ado, hata tukitenga *blocks*, wafugaji wadogo ni kama wajasiriamali wadogo ambao tunawapa mitaji kutokea Halmashauri, leo ndiyo imekuwa wanaonekana kero kwa sababu hawajaratibiwa vizuri. Ukipunguza kero unaongeza tija na ajira kwa watu wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia.

MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, yapo maeneo kwa kweli sisi kama Wabunge na wananchi tumeyaona, yakiwekewa mkazo vizuri tutaweza kufanya vizuri na tutakusanya pesa za kutosha. Kama hatutakuwa na mapato ya ndani ya kutosha, hatuwezi kupiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanahamisi. Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima atafuatiwa na Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

MHE. RASHID M. MTIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia mpango huu wa Serikali wa mwaka 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa namna walivyowasilisha huu mpango.

Wamejitahidi kuweka vitu wazi kabisa, na wameonyesha maeneo ya utekelezaji kwa robo ya kwanza. Kwa namna ipi tunalenga kwenye mpango wa muda wa kati na kuelekea kwenye dira, Wameonesha maeneo ya miundobinu ilivyotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa madini leseni 273 zenye vikundi 2,558 navyo vimehusika katika eneo hili la utekelezaji katika robo hii ya kwanza. Mali 48,713 zimerasimishwa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kuingia kwenye uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka nichangie katika eneo la kipaumbele namba sita, eneo ambalo linagusa misingi endelevu ya Taifa letu. Ninataka niende kwenye afua namba mbili na namba sita. Ni kwa namna gani tunaandaa Halmashauri zetu, na ni kwa namna gani tunaandaa wananchi kwenda kwenye kupanga mipango hii ya mwaka mmoja mmoja, mipango ya kati ya miaka mitano na kwenda kwenye dira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona utekelezaji wa robo hii ya kwanza, yako maeneo yameonesha kuwa mifumo imeanza kuandaliwa ya *e-Delivery,* utoaji wa taarifa ili tuone kwa namna gani tunafanikisha mipango hii. Mimi ninatamani sana kuona kuwa tunawaandaa wananchi katika hizi hatua za awali, tunaziandaa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afua namba mbili, ni mikakati gani thabiti tumeiweka kuweza kuziandaa Halmashauri, kuweza kuwaandaa wananchi? Kwa sababu, ukisoma maeneo ambayo mipango ya awali imeshindwa ni pamoja na eneo la udhaifu wa rasilimali watu na upungufu. Udhaifu wa rasilimali watu katika misimamo, mwenendo na mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, katika mipango hii tunayoileta sasa, ambayo sasa ndiyo tunaanza kutekeleza dira, sasa ndiyo tunaanza kutekeleza mpango wetu wa miaka mitano, maandalizi kule kwenye Halmashauri yako vipi? Je, wataalamu na Madiwani wanajua tunakoelekea? Wanajua malengo tunayojiwekea kwenda huko? Eneo hili ninatamani lifanyiwe upembuzi wa kina

kuona mipango hii tukiweka *a good landing ground* kule chini kwa wananchi ili iweze kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ndiyo wanapanga mipango katika *level* ya Halmashauri, wanatakiwa wajue, waelewe Madiwani na Watendaji wote waweze kuona kwa namna gani tunaandaa mazingira mazuri ya kutekeleza mipango yetu ya kati na ile ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mitizamo ya wananchi wetu tunawaandaa namna gani kwenda kutekeleza hii mipango? Tunaandaa namna gani maisha yao ya*-reflect* malengo ya Serikali kwenda kwenye miaka mitano, kwenda kwenye miaka 25? Nilitamani sana kuiona Serikali inafanya suala hili la kuandaa Halmashauri na wananchi katika mipango yetu ili udhaifu ule wa awali wa upungufu na udhaifu wa rasilimali watu katika kutekeleza mipango uweze kuondoka tunapoenda kwenye mipango hii ya awamu hii ya dira inaenda kwenye 2050. Hilo ni eneo mojawapo ambalo nilikuwa nataka nichangie kipaumbele cha sita lakini afua namba mbili na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni eneo la kipaumbele namba tatu kwenye afua ya kwanza, kuhusu upangaji wa miji. Nikiangalia eneo hili kipaumbele ni uhifadhi wa mazingira na namna gani tunakuwa himilivu katika masuala ya tabianchi. Ninatamani kuona eneo hili linaangalia upangaji wa miji na si tu kuweka mazingira mazuri. Ninatamani tuangalie eneo la upangaji wa miji kama eneo la uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunatambua ardhi ikipimwa wananchi wakapata hati, watatumia hati hizi kuweza ku*-access* mikopo. Ardhi ikipimwa inaongezewa thamani. Kwa hiyo, ardhi hizi ambazo leo wananchi wanazo, viwanja walivyonavyo mijini vikipimwa, thamani inaongezeka. Kuongezeka thamani ni suala la kiuchumi, kwa hiyo ninatamani tuangalie katika *angle* hiyo ya kuona kwamba upimaji wa ardhi iwe vijijini, iwe mjini ni suala la kiuchumi vilevile badala ya kuandaa tu mazingira bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala hili lina mapato ya Serikali, ardhi inalipiwa kila mwaka, ni suala la kiuchumi kuwezesha Serikali. Kwa hiyo, tukichukua fedha tukapeleka kwenye kupima vijijini, mjini, kwenye mashamba, tunaihakikishia Serikali kupata kodi mwaka kila mwaka. Kwa hiyo, ninatamani sana Serikali katika programu ya kupanga, kupima na kumilikisha, tutafute fedha tupeleke kule. Ninaona huu mradi kama unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua fedha kwenda kupima, kupima ni biashara. Tunaweza kwenda kukopa fedha hata benki tukapeleka kwenye kupima. Ardhi ikigawiwa watu wakilipia, si tutarudisha hiyo mikopo kuliko tunasuasua? Hata tuseme tu kwamba, basi mapato yanayokusanywa ya ardhi ya mwaka mzima yaachwe huko, Wizara ya Ardhi ipeleke kwenye Halmashauri wapime. Tukikamilisha tukahakikisha kwamba tunapata kodi ya kutosha, ndiyo iende ikatumike kwenye shughuli nyingine za za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninatamani Serikali tufanye maamuzi magumu ya kwenda kukopa au kuamua fedha zote zinazotoka kwenye sekta ya ardhi kama kodi, ziende tutumie kama *revolving fund* kwenda kupima miji yetu, kupima vijiji vyetu ili tujiimarishe katika kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka nichangie, niliipitia taarifa ya Kamati, imechambua vizuri sana, sana. Ninatamani kuiunga mkono Kamati eneo la barabara. Barabara zetu ni mbovu sana, imezungumzwa hapa barabara ya Mtwara – Mingoyo, vilevile imezungumzwa hapa barabara ya Mtama – Newala. Sisi tukifika Newala tunaenda mpakani Msumbiji. Mji wa Newala umechagizwa sana na biashara ya Newala na Mueda kule Msumbiji. Tukitengeneza barabara zetu kama hii ya kutoka Newala Mjini – Kiduni – Chihanga pale *Boarder*, wakati wote miji yetu hii ya pembezoni itafanya biashara. Hali ya barabara tuliyonayo leo ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninakwambia, mwananchi wa Msumbiji, Kaskazini mwa Msumbiji inategemea sana biashara Tanzania. Kutoka Dar es Salaam kwenda kupita Mtambaswala na

kupita pale Chihanga ni rahisi kupita Chihanga. Kwa hiyo, wakati mwingine ugumu wa kuzunguka mbali kwenda kuitafuta Dar es Salaam unafanya biashara kubwa isiwepo kati ya sisi na Msumbiji. Tunaomba kuwekeza nguvu kwenye barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la maji. Hapa ninaomba nizungumzie mradi wa Makonde. mradi wa Makonde hii ni bajeti, tunavyoenda mpango huu ni bajeti ya tatu, shilingi bilioni 84. Mara wameweka kwenye Mradi wa Miji 28, mara huku. Fedha hazipatikani. Tatizo ni nini? Tunaomba kama Kamati ilivyosema, miradi hii ambayo imeshaanzishwa itoke fedha tukamilishe kwenye maji, ili twende kwenye miradi mingine. Haiwezekani tuweke mradi miaka mitatu haukamiliki ule mradi wa Makonde. Unahudumia Newala Mjini, Newala Vijijini, Tandahimba, pamoja na Nanyamba; Halmashauri nne.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mtima.

MHE. RASHID M. MTIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilamtaja Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula ajiandae.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nijaribu kutoa mchango wangu kwenye mchango wa mpango, ambapo kwa kweli ninataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Kaka yangu Alexander Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri sana aliyoifanya kutuletea huu mpango hapa. Mimi ninataka nimwambie, mimi ni mwanafunzi wake wa nje ya darasa, tunajifunza mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninataka nimpongeze pia Mheshimiwa Spika leo ametupa somo zuri sana, huwezi kutekeleza mpango wowote kama huna *discipline* ya matumizi. Spika ametoa mwelekeo mzuri na hii iwe *spirit* ya kwenda nayo katika kutekeleza huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa na mambo matatu. Kwanza ni kuhusu msisitizo wangu kwenye kilimo, ninataka niiombe sana Serikali, kama tunataka kupiga hatua ni lazima tuweke nguvu kubwa sana kwenye kilimo. Kilimo kimechangia asilimia 19 ya *GDP* ya Taifa letu na hapo ni kilimo ambacho kilikuwa hakijapewa msukumo sana. Ninaiomba sana Serikali, tukiwekeza nguvu kubwa kwenye kilimo, kama tumepata asilimia 19 na hatujaweka msisitizo mkubwa, tukiweka msisitizo tukatengeneza mazingira mazuri ya wakulima wetu ninaamini kilimo kitatutoa kwenye asilimia 19 kutupeleka kwenye asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hiki ni vizuri Serikali ikakubali kupunguza mambo, tukaamua kupunguza vipaumbele. Tuamue kwamba tunakwenda na kilimo na mambo mengine, kilimo hadi sasa kimeajiri asilimia 65 hadi 70 ya watanzania, tukiweka msisitizo kama Taifa ni eneo ambalo kwa muda mfupi sana litatupa matokeo. Achana na hizi *PPP* ambazo watu kuja hadi wajifikirie, tunao watu huku ambao wanapungukiwa vitu vidogo sana, ambao wanahitaji msukumo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo Katavi, Tabora na Chunya tunalima tumbaku kwa wingi, hilo eneo lote hakuna kiwanda hata kimoja cha tumbaku. Tabora, Katavi na Chunya, wako kwenye eneo la *cycle* moja, kiwanda cha tumbaku kiko kimoja Morogoro. Kwa nini Serikali isitengeneze mkakati mahsusi wa kuweka kiwanda cha Tumbaku Tabora, ambako kutakuwa katikati au Katavi ili mkulima anayetoka Chunya, Katavi na Tabora aweze kuongeza thamani ya mazao yake hapo hapo katikati, kuliko hivi sasa tulivyo? Haieleweki mkulima wa tumbaku anauza tumbaku kwa shilingi ngapi. Kila siku zao linapanda na kuanguka kwa sababu hatujawekeza vizuri kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ninataka niwaambie Serikali, ifikie pahala tufanye *proper investment irrigation schemes*. Tukiwekeza kwa makusudi kwenye kilimo cha umwagiliaji, hapa hakuna stori. Kilimo kinataka kuwekezwa. Tukifanya vizuri kwenye kilimo cha umwagiliaji nchi zote ambazo zilipiga hatua kubwa sana kwa haraka waliwekeza kwenye kilimo. Ndiyo maana leo

tunawasifia China, tunawasifia Vietnam na maeneo mengine, waliweka nguvu kubwa sana kwenye kilimo cha umwagiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bwawa ninalo mimi pale Katavi tangu tume-*introduce* bwawa lile wamekuja wataalamu wanazunguka tu kama helikopta hawajui pa kutua. Kila siku ukiwauliza jamani bwawa langu la Ipwaga Masigo ni wapi? Hawaelewi wanatua wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima watu wawe *serious*. Ninataka nikwambie, nchi inatulia kwa sababu watu wanakula na kushiba. Tukiamua kung'ang'ana na kilimo kitatutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipongeze sana. Ziko baadhi ya kampuni ambazo zimefanya kazi kubwa, hapa ninataka niipongeze sana kampuni ya *NGS*. *NGS* hawa wanashughulika na kilimo cha pamba. Wanafuata wakulima walipo. Mkurugenzi wa *NGS* anakaa Simiyu lakini ameenda kutengeneza kiwanda Mpanda na ame-*introduce* kilimo cha pamba watu wanalima. Huo ndiyo mwongozo ambao tunataka Serikali iufuate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo mashine ya kuchenjua dhahabu unakwenda kutengeneza Mtwara ambako kuna gesi. Mashine ya kuchenjua dhahabu inatakiwa ikatengenezwe Geita na Chunya, Kwimba huko kwingine ambako wanachimba dhahabu. Sasa leo sisi tunalima tumbaku lakini sijui karakana za tumbaku ziko wapi. Wapi na wapi? Lazima tutengeneze mkakati, twende ili tupige hatua, o*therwise* hapa tutakuwa tunazungukazunguka tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote duniani ambalo lilitengeneza mpango ukatekelezeka ni lazima walikuwa wana *human capital*. Ili mpango wowote uende ni lazima uwe na vijana na uwe na watu ambao wako *committed*. Taifa hili asilimia 70 ni vijana. Tuna vijana wa aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea mara nyingi sana hapa. Leo hii kila unakozunguka ili upige hatua, wenzetu wote hawa China walipiga hatua kwa sababu vijana walikuwa wamepambana ili kuliondoa Taifa lao lilipo. Leo hivi tunavyoongea, kati ya vijana 10 sita wamelegea, halafu unasubiri upige hatua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *very serious issue*. Watu wanacheka Taifa liko kwenye *mzongemzonge*. Ukizunguka huko ukimuuliza Mama Gwajima anakwambia sijui Wizara ya Mambo ya Ndani, TAMISEMI, yaani sisi wenyewe tumechanganyikiwa. Vijana huko nje imekuwa shida. Taifa linapita kwenye mkanganyiko mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mpango huu utekeleze ni lazima tutengeneze mkakati wa kuwadhibiti hawa vijana. Kama hatuna mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba vijana wetu hawaharibiki, baada ya miaka 10, miaka mitano hatutakuwa na Taifa. Niwaombe sana Serikali, Taifa lolote lililopiga hatua liliwekeza kwenye nguvu kazi ya vijana. Sisi vijana wetu tumewaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukizunguka huko kila sehemu, wengine huko unakuta kesi nyingi mara huku sijui amelawitiwa, huku sijui amebakwa, mashoga. Hawa wanaolawiti, yuko Mbunge aliwahi kupendekeza hapa, kwa sababu, hawa wanaowalaiti vijana hawa ndio wanaotutengenezea mashoga huko mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko Mbunge aliwahi kutoa pendekezo hapa. Kuwa hawa wanaowalawiti na kubaka watoto, iletwa sheria hapa wahasiwe. Watu wakazunguka, wakalalamika, *issue* ikapita, leo *issue* ime-*backfire*. Taifa liko kwenye mkanganyiko. Hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, kama tunataka kuliweka Taifa hili vizuri ni lazima tuhakikishe kwamba vijana wetu wanakuwa kwenye mazingira mazuri. Niiombe sana Serikali, maeneo mengi sana; juzi wako vijana hawa ambao wananchi wanawahisiahisia kuwa wanashughulika na hayo mambo, nao wamelegealegea, walikwenda kule Mwanza; cha ajabu yaani

wale vijana wamepewa *escort* Mwanza kuliko hata Mbunge, hata Waziri akienda Mwanza hajawahi kupewa *escort*. Wametoka *airport* gari mbili za Polisi, mbele moja nyuma moja. Hakuna Waziri aliwahi kupewa mapokezi ya namna hiyo. Serikali, kwenye hafla zetu za Serikali za nini wanaalikwa. Wanakuja kufanya nini? Ili Taifa lipige hatua ni lazima tusi-*entertain* vijana wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninataka niishauri Serikali. Taifa hili lina mpango wa miaka 50 ni lazima tuamue. Moja, tuweke mpango mzuri kuanzia kwenye shule zetu, kutoka kwenye shule zetu twende kwenye vyuo ili kuandaa vijana kuja kufanya kazi za kulikomboa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga. Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, Mheshimiwa Haji Amour Haji ajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na nchi, kwa kunipa nafasi ya kusimama tena ndani ya ukumbi huu. Ninawashukuru sana wananchi wa Buchosa kwa heshima kubwa waliyonipa ya kuwa Mbunge wao. Ninaishukuru sana Serikali, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoendelea kutumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna wanavyoitumikia nchi yao na kupeleka Taifa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania nchi yangu ni Taifa ambalo Mungu amelipendelea sana. Ninakumbuka nimekuwa nikiamini mimi ni Taifa maskini, Tanzania ni nchi maskini, ni nchi ipo nyuma, ni Taifa linaloendelea. Mpaka siku moja nilipokutana na

Padri mmoja wa kizungu akaniambia, Eric usiyaamini hayo maneno yametengenezwa na wazungu ili kufanya Afrika iendelee kuwa katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni propaganda, hatukukutana mahali popote tukakubaliana sisi tuitwe ulimwengu wa tatu, hatukukaa mahali popote tukakubaliana sisi ni nchi maskini. Ni propaganda za nchi za magharibi kufanya Afrika na Tanzania iendelee kujiamini ni nchi maskini hivyo isipige hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ya Padri huyu yalinifanya mimi Eric, nijiamini na maisha yangu yabadilike kabisa. Ninatamka maneno haya nikiamini vijana wa nchi hii wananisikiliza huko walipo. Ninataka kuanzia leo watembee wakijiamini kwamba wapo katika nchi tajiri ambayo imebarikiwa sana na Mungu. Waache kuwa wanyonge, watembee wakiamini Taifa lao limebarikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi upo siyo maneno tu, nitakupa *data* chache, nilishazungumza, nitazungumza tena hapa. Nitazungumza kila ninapokwenda kwa dhahabu Tanzania ni nchi ya 20 duniani, kwa almasi Tanzania ni nchi ya 18 duniani kwa *helium gas* Tanzania ni nchi ya kwanza duniani, kwa *tanzanite* ni nchi ya kwanza duniani, kwa *natural gas* (gesi asilia) nchi ya 82, kwa makaa ya mawe ni nchi ya 52, kwa *graphite* ni nchi ya sita, na kwa *uranium* ni nchi ya 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utalii Tanzania katika Afrika ni nchi ya kwanza, duniani ni nchi ya pili ikiongozwa na Brazil. Taifa hili ni tajiri, limebarikiwa sana. Utajiri huu, sekta hizi zikitumika sawasawa Tanzania haiwezi kuwa tegemezi, sekta hizi zikitumika inavyopaswa, tukatumia utajiri huu kuubadilisha uwe fedha baadaye uweze kuleta maendeleo, Tanzania haiwezi kutegemea msaada kutoka nje, hiyo ndiyo imani yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana tumeishi kwenye kuamini sisi ni maskini, hatuna chochote, tunategemea msaada kwa watu ambao pengine tunawazidi hata uwezo. Tukikutana na mzungu mahali popote unaona msaada, huyo

mzungu mwenyewe anaweza kuwa masikini, amekusanya hela yake kwa mwaka mzima anakuja kutembelea Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *we are a rich nation*, *we are a wealthy country*. Tuache kutembea kinyonge katika nchi tajiri kama hii. Kazi yetu katika utekelezaji huu wa mpango huu kuelekea mwaka 2050, kazi yetu kama Taifa; kwanza, tuhakikishe sekta hizi zinachangia kwenye Mfuko wa Taifa. Sekta hizi zote zichangie kwenye Pato la Taifa, *GDP* yetu imejiwekea lengo la shilingi bilioni moja mwaka 2050. Hii inawezekana peke yake kama tutaweza kufanikiwa kubadilisha utajiri huu kuwa fedha na hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kwenye utalii. Utalii wetu ulikuwa unaingiza fedha kidogo sana, leo ninavyozungumza tunaingiza karibia shilingi bilioni tano kwa mwaka, kwa kucheza sinema moja tu *(royal tour)* watalii wamefurika hapa nchini. Ikifanyika hivyo kwenye madini, ikafanyika hivyo kwenye kilimo, ikafanyika hivyo kwenye sekta ya uvuvi, ninataka kukuhakikishia nchi hii itapiga hatua tena kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; amezungumza rafiki yangu Mheshimiwa Maganga, ili tuendelee tunahitaji kuwa na *skilled and informed powerful workforce*. Tuwe na vijana katika Taifa hili wenye uwezo wa kufanya kazi na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kupiga hatua, hatuwezi kutimiza malengo haya kama hatujawaandaa vijana wetu kupambana na vijana wa mwaka 2050. Elimu yetu tuipitie upya iwe ni elimu ambayo itamuandaa mwanangu kupambana na ulimwengu ujao. Malezi yetu sisi kama wazazi na kama Taifa tuwalee watoto wetu vizuri waweze kuwa *strong children* ambao watapeleka Taifa letu mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udumavu katika nchii hii, nilikuwa ninaongea na Mheshimiwa Naibu Waziri hapa. Udumavu ni 30%, watoto waliodumaa kwenye nchi hii ni 30%. Tafsiri yake ni nini?

Watoto waliodumaa wanakuwa na *permanent*, uwezo wao wa kujifunza unakuwa mdogo, ni *permanently* wamedumaa 30%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa 30% waliodumaa, mwaka 2050 watakuwa ofisini wanafanya kazi. Watoto wa namna hii wataweza kushindana na watoto waliolishwa vizuri? Tunaomba kama Taifa tuhakikishe kwamba lishe inafanyika na kilimo kinafanyika, Wizara ya Kilimo wazungumze na Wizara ya Viwanda ili kwamba mazao yetu yaweze kuwa na lishe na *nutrient* zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoyafanya haya, 2050 tutakuwa na watu ofisini, na Bungeni ambao uwezo wao wa kufanya maamuzi utakuwa mdogo, hatutashinda katika uchumi wa dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yasiyo ya kuambukiza *(non communicable diseases)* 30% ya vifo katika nchi hii kwa sasa vinatokana na magonjwa yasiyoambukiza. Watu wanaugua, nilikuwa Temeke hospitali juzi nimekwenda kutembelea hospitali, ninashangaa kwamba ugonjwa unaoua watu sana ndani ya nchi yetu sasa hivi siyo malaria, tulizoea malaria sasa hivi ni *hypertension*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *hypertension* inaongoza kuua watu. Watanzania wanaugua magonjwa haya yanakuwa mzigo mkubwa kwa Serikali. Sisi kama Taifa tuchukue hatua makusudi ya kuwafanya watu wetu waepukane na magojwa haya. Tusipofanya hivyo 2050 tutakuwa na Taifa la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Dar es Salaama sasa hivi tembea, *dialysis centres* kila kona watu wengi wanasafisha figo, figo zinakufa za vijana wetu. Vijana wetu wanaachwa wanakunywa *energy drinks* mfululizo, bodaboda wanakunywa *energy drinks* tano kwa siku, figo zinakufa tunaangalia hatuwasaidii vijana wetu. Tunasema ooh, tuna bima ya afya: bima ya afya ikizidiwa na magonjwa haya itakufa. Kama tunataka kuisaidia nchi hii tupambane na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na hapo ninakuhakikishia tutafika 2050 tutakuwa tumeshindwa na nchi ambazo zinachukua hatua leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kutoka kwenye *GDP* tuliyonayo sasa hivi mpaka *GDP* ya *one trillion*. *One trillion* siyo kazi ndogo tusidanganyane, lazima watanzania tujue hii ni vita. Mwaka 1978 baada ya vita vya Uganda Mwalimu Nyerere alitamka maneno akasema nilikuwa mdogo, tufunge mikanda kwa miezi 18. Watanzania lazima tuelewe hii ni vita na kama ni vita kila mtu ajue tunapambana kutoa nchi yetu kwenye umaskini, wananchi waelewe na sisi viongozi tuelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yetu yote yatakayofanyika hapa ndani yawe ni maamuzi ya kizalendo kwa faida ya nchi yetu. Kama hatutafanya hayo, tutapanga mipango mizuri, watakuja watu wasiowaaminifu, pesa zitazidi kuibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana pia tushughulike na suala la *monitoring and evaluation*. Fedha zinapotea, huko kwangu Mtendaji kala hela ya Mfuko wa Jimbo, tumewekana ndani. Je, mambo haya yanafanyika kila sehemu? Sisi kama nchi *monitoring and evaluation* ninaomba sana iimarishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia. Kama haitakuwa Wizara iwe mamlaka ili kwamba kuwe kuna watu ambao wanaamka kila siku kwenda kufuatilia fedha zetu na iwe chini ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ahsante kwa kunipa nafasi Mungu akubariki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Eric Shigongo kwa mchango wako mzuri. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo ajiandae.

MHE. MARIAM A. MUNGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nipate kuweka

mchango wangu kidogo katika Mpango wetu huu wa Maendeleo wa mwaka 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika sekta ya nyumba na maendeleo ya makazi. Kwanza ninaomba niipongeze sana Wizara ya Mipango kwa kuja na Mpango mzuri Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na timu yake yote, niwaombee wao na watekelezaji wote ikiwemo na sisi, Mwenyezi Mungu atuwezeshe ili tuweze kutekeleza Mpango huu na nchi yetu iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa unapaswa kuwa ni hatua muhimu sana katika kutekeleza ahadi za Chama cha Mapinduzi ambacho ndiyo Chama kinachoongoza Serikali yetu na ndiyo Chama kimeshika hatamu na kiliahidi wananchi. Sasa Mpango huu unatakiwa ndiyo uwe hatua muhimu katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2025 -2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kunukuu kidogo kwenye ukurasa wa 27 wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2025 - 2030 kwenye sekta ya nyumba na makazi. Ilani inasema kwamba, imeahidi Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa wananchi kuchukua hatua zifuatazo: hatua ya kwanza, "kutunga na kutekeleza sera ya nyumba na makazi itakayokuwa dira ya maendeleo ya sekta ya nyumba na makazi nchini"; halafu ikaahidi tena hatua ya pili kwamba, "kutunga na kutekeleza sheria, kanuni na mikakati itakayosaidia kupunguza gharama za ujenzi ili wananchi wa kipato cha chini waweze kujenga nyumba za kisasa na kwa gharama nafuu. Lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030, Serikali inajenga na au kuwezesha ujenzi wa nyumba bora na za bei nafuu zisizo pungua 50,000".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi hizi zimeendelea zipo kama ahadi nane ikiwemo ahadi ya saba ambayo inasema, "kutekeleza programu maalum ya ujenzi wa nyumba kwa makundi maalum ya watumishi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye vipaumbele vya mpango wetu wa mwaka 2027/2028 katika mageuzi ya sekta za kimkakati, mpango umeainisha hatua kadhaa katika maendeleo ya makazi zikiwemo kuimarisha usimamizi wa ardhi, kuendeleza miji na kupanua upatikanaji wa fedha za ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia tena huu Mpango, kwa bahati mbaya sijaona; kule kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi wameweka idadi kamili kwamba mpaka tutakapofikia mwaka 2030 tunatakiwa kuwa tumejenga nyumba 50,000 ambazo sasa hivi ukiangalia huu Mpango tupo Katikati ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya 2025-2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *by the time* huu Mpango unapoishia mwaka 2028 tutakuwa tumeshafika katikati. Mimi nilikuwa ninategemea kwamba katika Mpango kuwe kunaoneshwa takwimu angalau za kila mwaka kwamba ili kufikia ile idadi ambayo tumeiahidi mwaka huu tunajenga nyumba 10,000 au tunajenga nyumba 15,000, 25,000 *and so forth* mpaka zitakapofika hizo nyumba 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema inataka kuweka kwenye utekelezaji kuhusiana na ujenzi wa nyumba za bei nafuu. Katika Mpango wetu kwenye suala zima la nyumba za bei nafuu nimepitia na kuangalia kwamba tunaweka nguvu kubwa au tunaipa uwezo mkubwa shirika au taasisi ambazo ni za kiserikali ndio ziweze kujenga au tunaipa hili jukumu la kujenga nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nyumba 50,000 siyo chache na mpaka sasa hivi kwenye Serikali sisi tunategemea zaidi kwa mfano Shirika la Nyumba la Taifa katika kujenga hizi nyumba za bei nafuu lakini ukweli ni kwamba, Shirika la Nyumba la Taifa lilikwisha hama huko katika kujiendesha au kujenga nyumba za bei nafuu, linajiendesha kibiashara kwa sheria ya mwaka 1990.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Shirika la Nyumba la Taifa ni sawasawa na *contractor* mwingine yeyote aliyopo mtaani

anayejenga nyumba za kibiashara na kuuza. Isipokuwa yeye anaacha asilimia kidogo sana kwa kuendeleza ile *public housing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara ya Mipango, kwa sababu Wizara ya Mipango ndio Wizara mtambuka na imesimamia huu Mpango wetu. Kwenye hili suala la kuwa na sera kama ilivyoelekeza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Ilani iliona umuhimu sana wa kuwa na sera *specific* ya nyumba na ndio ikaiweka kama ndio hatua ya kwanza katika mipango yake ya kutekeleza kwa hichi kipindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakuwa nyuma sana, mimi nilitegemea kwamba kabla hatujaanza kupanga mipango hii mingine yoyote tuwe na sera *in place* ambayo inafanya kazi na haya mambo mengine yote yangekuwemo ndani ya ile sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatujachelewa, niombe sana Wizara yetu ya Mipango ninyi ndio m-*take lead on this* kwa sababu kwa kuwa ninyi ndiyo Wizara mtambuka mtaweza kufanya kazi na Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Ardhi ili sasa tuje na sera ambayo itapelekea na sheria ya ardhi itakayotusaidia sisi kuweka mipango yetu hii sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua katika Wizara yetu ya Katiba na Sheria tuna ile Tume ya Kurekebisha Sheria inayoendelea na zoezi la kuziweka sheria zetu, ku-*harmonize* sheria zetu ili ziendane sawa na dira yetu ya Taifa ya 2050. Hili halipo kabisa tuna *gap* ya hii sheria hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri nikuombe sana tulichukue tulisimamie tulifanyie kazi kwa sababu bila ya kuwa na hiyo sheria hatutakuwa na maendeleo yoyote, hakuna kitakachokuwa kinaendelea cha msingi katika hii mipango yetu yote mizuri tuliyonayo ya sekta ya nyumba itashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimesoma tumeweka kwa mfano, kupunguza gharama za ujenzi. Sasa tutapunguzaje gharama za ujenzi wakati kila asubuhi akiamka mfanyabiashara anajiongezea bei? Sisi nchi hii tuna viwanda zaidi ya vitano sijui vya *cement* na malighafi zote za *cement* zinatoka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia mchangiaji mmoja juzi akisema kwamba, kuna maeneo wananunua *cement* kwa shilingi 40,000, sasa hii hatutaweza kufika bila ya kuwa na usimamizi, lazima tuwe na *checks and balances*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tu, mimi nilikuwa na mwalimu wangu mmoja ambaye amenipa msingi wa maisha wa *high school,* Mwalimu wangu Mkuu, alikuwa kabla ya mitihani anatuweka *assembly* asubuhi anatuambia, *remember the five Ps*, kama haujasoma utafeli. *Five Ps* zake anakwambia ni *prior preparation prevents poor performance*. Kuwa na sera ya nyumba na makazi itakayopelekea tuwe na sheria ya nyumba na makazi, hiyo ndiyo *preparation* yetu ya maana na bora itakayotufikisha tunapotaka kuelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mariam. Nilimtaja Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel ajiandae.

MHE. HAJI AMOUR HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Dunia kwa kuweza kutuwezesha kuwemo humu na kuendeleza shughuli zetu za kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji kwa kuweza kutuletea taarifa hii ambayo inaonesha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kabla ya kuchangia asubuhi hapa baada ya kufika ndani ya Bunge hili tulipewa taarifa ya kudhibiti matumizi ya mapato hasa katika vyombo vya moto na mambo mengine hasa kwa watendaji wetu ambapo taarifa ile ilitolewa na Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ukumbusho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kupitia Wizara ya Mipango kama ingewezekana mambo yale yote nayo yawe kama ni moja ya mapendekezo na yaingizwe kwenye mpango ili kujua huko tunakokwenda lengo letu kubwa hasa tunatakiwa tufikie katika hali gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine juu ya taarifa ile ambayo imetolewa si mara ya kwanza wala mara ya pili, labda katika mchango wangu niseme tu kwamba taarifa ile ingependeza pengine iwe kama ni Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusudi huko nje wafahamu wazi kwamba Wabunge wameazimia kitu gani hasa cha upunguzaji wa matumizi pamoja na mambo mengine ili kusudi Taifa letu liweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika mchango wangu niseme tu kwamba lengo la mapendekezo ya mpango ni kupunguza umaskini. Tunapozungumza kupunguza umaskini kuna nyanja kubwa. Katika umaskini kuna hali kubwa sana tunaposema kwamba tunapunguza umaskini, kuna ule umaskini wa kipato, umaskini wa njaa, umaskini wa maradhi kwa kila namna ambavyo ilivyo na kwa namna ambavyo mpango wetu huu ulivyojikita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba Mpango wa Maendeleo haupaswi kupimwa kwa idadi ya miradi iliyopangwa pekee bali kwa uwezo wake wa kuongeza uzalishaji. Tukizungumzia suala la uzalishaji, ni aina ya jambo ambalo ni kubwa sana. Watu wote ambao wanasimama hapa utasikia kwamba tuboreshe kilimo chetu, tuboreshe mifugo yetu, lakini ukiangalia hayo yote ni kama ni sehemu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia aina kuu za uzalishaji utakuta kwamba kuna uzalishaji wa kilimo, lazima kilimo chetu kiwe bora; tuhakikishe kwamba tunalima mazao ambayo ni ya biashara; tuna mifugo ambayo ni ya biashara; tufanye uvuvi ambao ni wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tuwe na uzalishaji wa viwandani. Tuhakikishe kwamba ndani ya viwanda vyetu tunapata malighafi za kutosha. Ninatumaini kwamba kwa Tanzania kama tunaweza kujipanga hasa, si kama kwamba hatuna rasilimali za viwandani lakini shida ni namna tu ambavyo tunaweza kuzitumia hizo rasilimali za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ni uzalishaji wa huduma ambalo linachukua nafasi kubwa sana. Tukizungumzia kwamba uzalishaji wa huduma humo ndani kuna suala la usafiri, kuna suala la la utali, kuna suala la elimu, afya, na huduma za kifedha. Tukizungumzia suala la uzalishaji tena, tuna suala la uzalishaji wa maarifa. Maana yake maarifa nayo ni moja ya sehemu ya uzalishaji. Tukizungumzia uzalishaji wa maarifa maana yake lazima kutengeneza zile tafiti zetu, tuzalishe tafiti zetu. Tuhakikishe kwamba tunakuwa na teknolojia ya kisasa pamoja na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu kwamba pamoja na yote tumezungumza masuala mengi sana ambayo lengo ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inakua na uchumi wetu unakuwa himilivu. Ukiangalia mipango siyo shida, tuna mipango mizuri sana na ninaisifu sana mipango ambayo wanatuletea Wizara yetu ya Mipango. Hongereni sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa namna ambavyo umetupatia mipango yetu, lakini shida ambayo inakuja alizungumza pale mchangiaji mmoja kwamba shida yetu inakuja kwenye suala *mindset* pamoja na *attitude*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ukizungumzia *mindset* na *attitude* maana yake inawezekana ikawa ni tatizo kwetu. Tuna kila kitu, tuna rasilimali nyingi ambazo zimetajwa lakini kwa nini kama nchi hatupigi hatua ile ambayo tunaikusudia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda pengine kwa yote ambayo yanafanyika katika mipango labda nije na ushauri hasa kwa upande ule wa *monitoring and evaluation*. Kitu chochote bila ya ufuatiliaji na tathmini ni ngumu sana kuweza kufika. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yetu yote ya maendeleo ya Serikali ili

kuhakikisha kuwa miradi yetu inatekelezwa kwa malengo yaliyokusudiwa kwa wakati na kwa thamani halisi ya fedha za umma zilizowekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto si fedha tu au kuanzisha miradi pekee bali ni kuhakikisha kuwa miradi hiyo inazalisha matokeo yanayopimika na kuleta tija ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Bila ya hivyo maana yake hatuwezi kupiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme tu kwamba kila mradi katika pendekezo langu uwe na viashiria mahsusi vya utendaji *(KPIs)* vinavyoashiria hivyo vioneshe matokeo yanayotarajiwa, gharama za mradi, muda wa utekelezaji, idadi za ajira zinazozalishwa, mapato yanayotarajiwa, na mchango wake katika uzalishaji wa Taifa. Viashiria hivi vianze kabla ya mradi kuanza ili kurahisisha kutathmini matokeo. Bila ya hivyo tutakuwa hatuwezi kupiga mbele hasa kwenye suala la ajira hizi za vijana. Ikiwa kila mradi tuna tathmini ajira ngapi zimepatikana na tukazisema maana yake kidogo tutakuwa tunaona ile hatua ya ajira ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije na ushauri mwingine ambapo niseme tu kwamba Bunge lipewe taarifa za matokeo badala ya taarifa za matumizi pekee. Taarifa za Serikali ziainishe si fedha tu zilizotumika tu bali malengo yaliyofikiwa na ambayo hayajafikiwa, sababu za mapungufu, na hatua ya kuyatatua. Kwa sababu bila ya Bunge kuweza kutathmini itakuwa ni shida

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme tu kwamba waswahili wanasema kwamba "Mipango si matumizi." Matumizi ni yale ambayo unayokusudia kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niseme tu kwamba mipango yetu lazima iendane na bajeti zetu ili kuweza kupiga hatua, isiwe tuna mipango bila ya bajeti. Tukikosa mipango bila ya bajeti maana yake hatuwezi kufika pahala popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme tu kwamba ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Haji Amour Haji. Nilimtaja Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo atafuatiwa na na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel. Mheshimiwa Kafiti William Kafiti ajiandae.

MHE. IBRAHIM M. SHAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia Mpango wa Serikali 2027/2028. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia sote afya na uzima wa kuweza kuiona siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia sote afya na uzima wa kuweza kuiona siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nyingi anazozifanya katika nchi yetu. Vilevile, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kuwachagua na kuwateua hawa Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwateua na kuwachagua hawa Mawaziri na kupewa dhamana kubwa ambayo wanayo ni kazi kubwa sana. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu, Mheshimiwa Profesa Kitila. Mimi si mwalimu wangu kwa sababu elimu yangu mimi ni ndogo ni kidato cha nne lakini nimemzidi Mheshimiwa Musukuma Darasa la Saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba 75% ya ardhi katika nchi yetu haijapimwa. Ardhi iliyopimwa ni takribani 15% mpaka 25%, lakini hii 75% sasa tunataka tuone kwamba katika huu mpango unasisitiza jinsi gani ya kuweza kuhakikisha kwamba inakwenda kupimwa ili Watanzania waweze kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo faida nyingi sana za Watanzania kumiliki ardhi kuwa na hatimiliki. Faida kubwa ni Mtanzania kujisikia kwamba ana-*own* (anaweza kumiliki) lile eneo, lakini faida nyingine kwa kupimwa na kupata hati kunamsababishia Mtanzania aweze kupata mikopo kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi benki hazipendi sana kuchukua makochi lakini wanapenda sana kuchukua hati na kuweza kuwafanya Watanzania wapate mikopo. Nilitamani tuje na mpango wa ardhi maghorofa. Ardhi maghorofa maana yake ni kwamba katika nchi yetu yako maeneo *potential* sana. Ukienda Dar es Salaam, Oysterbay na Masaki ukirudi pale Moshi Mjini kuna maeneo ya *Shanty Town* eneo moja sasa hivi la kiwanja karibu milioni 500 bilioni, moja bilioni mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunahitaji kwamba watu wa ardhi sasa waende kwenye yale maeneo, kama eneo *potential* lile liweze kupata hati. Kama ni eneo linafaa kujenga ghorofa 10 basi apate hati 10 kwenye lile eneo. Tunafahamu mpango wa nchi nchi yetu kwamba tuna uwezo sasa hivi wa kujenga nyumba ghorofa 10 na ukaweza kuziuza *apartments,* ukauza ghorofa ya kwanza, ghorofa ya pili; hilo lipo na linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa tuje na mpango wa kwamba ukiwa na kionjo chako ambayo ni eneo *potential* watu wa ardhi (mipango miji) waweze kutupatia hati, ghorofa 10 tupewe hati 10 ili anapokuja Juma tuweze kumuuzia ghorofa ya kwanza, ghorofa ya pili, ghorofa ya tatu, ghorofa ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *foundation* lazima iwe ghorofa 10 na *foundation* ataifanya yule mwenye kiwanja kwa kujiunga na *PPP* na kuingia katika mikopo ya benki zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo itasaidia sana kwamba sasa hivi wenye ardhi zile ambazo ziko *potential* wanauza zile ardhi na kurudi vijijini na hatimaye wanakuwa maskini. Tunapowapa nafasi ya kuwa na ile ardhi na kuwapa kumiliki ghorofa 10 ina maana hata wao kurudi kijijini hawatarudi. Watauza ghorofa ya kwanza, ya pili, ya tatu na hatimaye maisha yataendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la viwanda. Sera ya Tanzania ni ya viwanda na hii Sera ya Tanzania ya Viwanda ndugu yangu, Profesa ninaona kama vile sasa inakufa. Tunapewa mipango kwamba nchi itakuwa na viwanda lakini tuje na mipango ya kwamba pale Mwanza tutakuwa na kiwanda cha bilioni kadhaa, kitajengwa kiwanda cha samaki. Pale Tabora kutakuwa na kiwanda na kitajengwa kwa thamani kadhaa. Pale Mtwara kutakuwa kuna kiwanda cha korosho na kitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwe na mipango siyo tutajenga viwanda. Kweli hata ilani yetu inasema tutajenga viwanda kuanzia wilayani, mikoani lakini sasa mipango kwenye mpango uje mpango. Kwa mfano, sisi watu wa Moshi pale Moshi mjini tuna maeneo makubwa ambayo watu walimiliki kwa ajili ya viwanda lakini viwanda vile haviendelezwi. Sasa zile ardhi na yale maeneo ya viwanda tuje na mpango kwamba lile eneo la pale Mwanza Serikali itatengeneza kiwanda cha samaki chenye thamani ya kiasi fulani. Pia, katika mwaka huu tutajenga viwanda kadhaa wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unapojenga viwanda tuna-*create* ajira nyingi sana. Vilevile, tunayapa thamani yale mazao ambayo yanatoka kwenye ile mikoa. Tunakuwa tunaweza kushindana na soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona viwanda vingi sana vinajengwa Bagamoyo na Chalinze, ile ni kasumba tu, lakini watu wa Katavi, watu wa Bukoba, watu wa Shinyanga, watu wa Kagera pia viwanda vile vinaweza kujengwa kule siyo kuwekeza viwanda mahali pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawekeza viwanda mahali pamoja kwa kigezo kwamba bahari iko karibu, usafirishaji utakuwepo utakuwa rahisi. *No* twendeni Katavi, twendeni kule Bukoba, twendeni Shinyanga, Singida tuwashawishi, Simiyu tuwashawishi wale wawekezaji kwa kodi. Huenda mtu anayejenga kiwanda Bagamoyo analipa kodi 100% sasa mtu yule

akienda Simiyu alipe kodi 50%. Kwa kufanya hivyo tuta-*create* wawekezaji wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee suala la stendi. Zamani kulikuwa kuna stendi kule Kisutu lakini ikatoka Kisutu ikaenda Ubungo. Inaenda yenyewe yaani mahitaji yanahitaji yenyewe, kwamba mji unakua, watu wanaongezeka tukahamia Ubungo lakini baadaye tukatoka Ubungo tukahamia Mbezi Magufuli na tutegemee kabisa miaka inayokuja tutatoka Mbezi tutahamia mpaka huko Chalinze na wapi na wapi. Hii inaonesha jinsi gani mji unakuwa mji unapanuka, Watanzania wanaongezeka na watu wanafanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuje kwenye mpango sasa wa kuhakikisha kwamba kwa mfano watu wa kusini kule, Mtwara, Lindi, Masasi siyo lazima tuje kwenye stendi ya Magufuli. Twende tukatengeneze stendi kubwa ya kifahari kule Temeke kule ili watu wafanye nini? Watu wa kule watoke kule waende kule. Hata huu mgogoro unaosikia wafanyabiashara wa mabasi utakwisha. Tunajua watu wa Mwanza, watu wa Mwanza tujenge stendi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia sana na hizi stendi ambazo zimeshajengwa. Kwa mfano, Moshi ipo stendi ambayo nchi imetumia hela nyingi sana, pale stendi imetumika zaidi ya bilioni 18 iko zaidi ya 85% sasa hivi imebakia 15% ile stendi; ni kubwa ya *East Africa* nchi imetumia *a lot of money* pale. Sasa tufike mahali stendi kama hizi ambazo nchi imetumia hela nyingi hebu katika mpango Mheshimiwa Waziri aone kabisa kwamba pale sasa nchi imewekeza hela nyingi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye mpango wetu tuhakikishe stendi zile za Mkoa wa Kilimanjaro, Tabora, Shinyanga, Simiyu zinakwisha. Lazima tutanue wigo na Mpango utuoneshe na hizi stendi siyo lazima tutumie fedha zetu za Serikali. Tutangaze *PPP,* tutangaze wako wafanyabiashara wa ndani na wa nje ambao wana hela nyingi sana, tutangaze, tutakapotangaza huu mpango watu watawekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa *National Housing,* wenzetu wa *TBA* wana viwanja ambavyo viko *very potential*. Kwa mfano, pale Moshi *TBA* katikati ya mji wana eneo la eka zaidi ya 30 watangaze watu waingie *PPP* pale, tuoneshe mipango. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Mipango onesha mipango ya wazi kwamba ndani ya kipindi hiki tutafanya moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimshukuru lakini nimwombe sana Mheshimiwa Mpango kwa heshima kubwa na Mheshimiwa Profesa Kitilia nimwombe sana kwamba aoneshe mipango ya wazi na atueleze ili baada ya mwaka mmoja tuje tuulize kwamba alituambia kutakuwa kuna kiwanda Simiyu kiko wapi? Alituambia kutakuwa kuna kiwanda Lindi, Rukwa kiko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda na hizi hadithi kwa mfano tarehe 1 Juni, mliniambia mimi Mbunge wa Moshi Mjini kwamba kuna barabara ya njia nne itatoka Maili sita kupita Kiboroloni – Shatuwaz. Kwa kweli nilikwenda nikawaambia wananchi wakae mkao wa kula, wakae mkao wa kupata maendeleo. Barabara ile inakuja inasainiwa tarehe 1 Juni. Tarehe 1 Juni imefika wananchi wananizomea, Mheshimiwa Mbunge vipi kauli yako tena umeiongelea ndani ya Bunge Tukufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawaambia bwana subiri nimeambiwa Tarehe 1 Oktoba, Tarehe 1 Oktoba imefika ninaambiwa Tarehe 1 Novemba. Tarehe 1 Novemba ni kesho ninasubiri. Tufike mahali hata sisi Waheshimiwa Wabunge mnapotuambia kwamba kitu hiki kinatokea katika Majimbo yenu mwezi gani, siku fulani kama hakuna uhakika tusiseme.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. IBRAHIM M. SHAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo kwa mchango wako mzuri. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt.

Godwin Oloyce Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mheshimiwa Emmanuela Mtatifikolo ajiandae.

Mheshimiwa Kafiti William Kafiti.

MHE. KAFITI W. KAFITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo kwa kuendelea kutujalia afya njema. Vilevile, ninaendelea kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuisimamia nchi yetu na kuhakikisha inapiga hatua katika maendeleo. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yote ya Wizara kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela, nichangie Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/2028. Utekelezaji wa mpango ni jambo moja, lakini ni kwa namna gani tunakwenda kuutekeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mipango mingi sana huko nyuma, lakini tukiulizana ni hatua gani tumezichukua kuhakikisha mipango hiyo inatekelezwa kwa mujibu wa makubaliano? Tumekuwa tukiipanga mipango mingi, lakini inapokuja kwenye suala la utekelezaji, mambo yanakuwa ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *point* yangu hapa ni nini? Tunapopanga jambo, ni lazima tukubaliane, ni lazima tupeane muda, na lazima tupeane ni lini na wakati gani mradi huu tunakwenda kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mambo mazuri sana kwenye huu mpango, lakini sasa tunaangalia utekelezaji wake ni kweli una mashiko? Una vitu vingi vizuri sana. Ninaweza nikasema mpango ni sawa na ndoto ambayo tunategemea baadaye ije kuwa ndoto ya kweli. Kwa hiyo, haya tuliyotajiwa kwenye mpango huu, kama kweli yatazingatiwa na Wizara hii,

yatazingatiwa na Serikali, basi ninaamini Taifa letu linakwenda kupiga hatua mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, nishauri tuwe na mapitio ya mipango hii ambayo tunaipanga kila wakati. Tuna mipango ya nyuma huko, tukiulizwa leo tumeifanikisha kwa asilimia ngapi? Hatuna majibu. Sasa, ninaomba sana tunapomaliza kwa mfano Mpango huu wa 2026/2027 kabla ya kwenda Mpango wa 2027/2028, tupewe utekelezaji wa mpango uliopita ili tujue ni kwa kiasi gani tumefanikiwa kutimiza malengo ya mpango huo. Tofauti na hapo, tutakuwa tunakuja hapa, tunapiga mipango yetu, tukifika mbele hakuna tulicho-*achieve*. Kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mpango unatakiwa tuwe na fedha. Wenzangu wametoka kusema hapa, ukiwa na mpango huna fedha ni sawa na kazi bure. Ni lazima tuwe na fedha. Sasa, Serikali inapotuletea haya pamoja na kufanya hizi *PPP* yenyewe, ni lazima iwe na bajeti ya kuhakikisha inakwenda kutekeleza mpango huo. Kama hakuna, tutakuwa tunapiga *story* tu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuna wawekezaji wazawa wengi. Sasa ni wakati wa Serikali kuanzisha kitu kinaitwa *National Investment Fund* kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji wazawa. Leo wawekezaji wazawa wanapambana kujikwamua kiuchumi, lakini Serikali inawashika kwa namna gani? Je, wawekezaji wana uwezo wa kupambana na kampuni za kigeni kukamilisha miradi hii? Je, wawekezaji wana namna gani ambayo Serikali inawawezesha ili waweze kushindana? Leo tunaona kampuni nyingi hapa za madini zina uwekezaji mkubwa zaidi ya shilingi trilioni za kutosha, lakini ukiangalia ushindani wetu wa kampuni za wazawa na hizi za nje, unakuwa ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi kama China, China ina wafanyabiashara wake wazawa, inawapa mitaji kwenda kushindana na Mataifa mengine. Sisi hapa Tanzania Serikali imewawezesha watu gani? Tunaiomba Serikali iwe *backup* ya

wafanyabiashara na wawekezaji wa nchini ili kuleta tija kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Dira ya 2050. Tumesema nchi kama nchi inatakiwa tuwe na pato la dola trilioni moja na pato la mtu mmoja mmoja dola elfu saba. Sasa tujiulize, hili pato la trilioni moja kama hakuna mazingira mazuri ya kuwawezesha hawa wazawa hatuwezi kulifikia. Ni lazima tuje na mpango wa kuwekeza katika viwanda, tuje na mpango wa kuwekeza katika kilimo. Tumeona hapa pato la Taifa zaidi ya 19.5% limechangiwa na eneo la kilimo, zaidi ya 16% limechangiwa na eneo la fedha na bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba sana katika hili, ili kufikia hilo pato, ni lazima tuimarishe viwanda vyetu vya ndani, na ni lazima tuimarishe kilimo chetu. Tukiimarisha viwanda na kilimo, uzalishaji huu wa mazao ya kilimo utakwenda kuwa msaada mkubwa wa kulisha viwanda vyetu. Vilevile, tuache kufanya *export* ya *raw material.* Ni lazima tuhakikishe sasa tunasafirisha zile *final goods* ili nchi iweze kupata mapato mazuri na fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nijikite hapa hapa kwenye kilimo. Tumekuwa tukisema kilimo ni uti wa mgongo, lakini kwenye Dira hii sijaona ikisema imewaandaaje vijana kwenda kutimiza ndoto za Dira hii. Tuna vijana wengi ambao wako mtaani hawana ajira. Ninaomba sasa Wizara ije na mpango wa kuhakikisha vijana hawa wanakwenda kuhakikisha Dira hii na ndoto hii ya 2050 tunakwenda kuitimiza. Ni lazima kama Taifa tuwekeze kwa vijana ambao ni zaidi ya 60%. Sasa Dira hii kama hakuna mpango wa kuwawezesha vijana kutimiza ndoto hii itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ihakikishe tunawatumia vijana hawa, tuhakikishe tunaandaa mazingira mazuri ili vijana hawa waweze kupata ajira. Vijana hawa wakipata ajira, maana yake ule uchumi wa mtu mmoja mmoja wa dola 7,000 ambao Dira unasema 2050, tutakwenda kuufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye suala la ukuaji. Tumeona kwamba kufikia 2026 tutakuwa na ukuaji wa asilimia sita nukta tatu. Bado ninarudi palepale, ni lazima Serikali itengeneze mazingira mazuri ya kufanya uwezeshaji, vilevile kuhakikisha zile *informal business* tunazirasimisha, kwa sababu ukiangalia, wengi hapa zaidi karibu asilimia saba ndio wamesajiliwa kwenye hii *informal sector*. Zaidi ya 97% sasa tuombe sana kupitia Wizara hii ya Mipango iangalie Wizara za kisekta iweze kurasimisha hizi *informal sector* ili nchi na Serikali iweze kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, kwa sababu tunakwenda kwenye uwekezaji wa *PPP,* ni lazima sasa Serikali iweke mazingira mazuri ya kuaminika na hawa wawekezaji wa ndani. Tumeona wawekezaji wazawa wamekuwa wakipambana kujikwamua, kufanya uwekezaji; tumeona miradi mingi hasa miundombinu Serikali inawapa miradi hiim lakini suala la kuwalipa imekuwa kizungumkuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunataka wawekezaji wetu wa ndani, au wafanyabiashara wetu wa ndani, au wakandarasi wetu wa ndani ili waweze kupiga hatua na kufikia dira tunayoitaka, Serikali iweke mazingira ya kuwalipa kwa wakati ili kuondokana na madeni na mzigo mkubwa wa kwenda kufilisiwa na benki hizi. Kwa hiyo, ninaomba sana katika eneo hili Serikali iweze kuweka mkazo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Dira hii haiwezi kutekelezwa na Wabunge tu humu ndani na Serikali peke yake ni lazima iwe na ushirikishwaji. Ni lazima iwe na ushirikishwaji wa wananchi, Madiwani pamoja na halmashauri zetu ili tuweze kuimba wimbo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mmeona hapa juzi tumekuwa na elimu kubwa ya *El-Nino,* hata mtoto mdogo leo ukimwuliza anajua kuna *El-Nino* inakuja. Sasa elimu hii ya Dira iende itambae mpaka kule chini ili kila mmoja aimbe Dira moja. Malengo ya 2050 ya Serikali yenye matumaini mapya, Serikali yenye tabasamu kwa wananchi wake ni lazima

tuyatimize. Dira hii ni ya msingi kwa maendeleo ya nchi yetu na ni lazima tupige hatua kwa pamoja. Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kafiti Wiliam Kafiti. Nilimtaja Mheshimiwa Emmanuela Mtatifikolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, tutamalizia na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Waheshimiwa Wabunge, tumeongeza muda tuweze kumaliza shughuli ambayo iko mbele yetu.

MHE. EMMANUELA K. MTATIFIKOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Mpango huu wa Maendeleo 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anatuongoza vyema. Pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wetu wa Mipango, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo pamoja na timu yake nzima kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutengeneza mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuungana na wenzangu wote ambao wamechangia kwenye mpango huu, lakini nitajikita moja kwa moja kwenye eneo moja ambalo tumeona wote kwa pamoja kwamba limekuwa na matokeo makubwa ya kuweza kusukuma uchumi wetu, nalo siyo lingine ni kwenye eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kila anayesimama hapa anazungumzia kilimo, kila anayesimama anazungumzia kilimo, hii si bahati mbaya. Ni kwa sababu, pia tukiangalia kwenye nchi nyingine za wenzetu ambao walikuwa kwenye *level* moja ya maendeleo na sisi, na wengine walioweza kuinuka kwa haraka, wengi waliwekeza kwenye kilimo, kwa mfano tukiangalia *Vietnam*, *India* na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hili na sisi kwa upande wa Tanzania tunatakiwa kuhakikisha kwamba tunajiweka vizuri. Tukiangalia, tuna ardhi nzuri yenye rutuba, lakini tuna maji ya kutosha, tuna rasilimali watu ambao ni vijana wa kutosha wa kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la kilimo niipongeze sana Serikali, kuna uwekezaji mkubwa ambao umeshafanyika mpaka sasa. Tumeona mbolea za ruzuku zinatolewa, tumeona Maafisa Ugani wameandaliwa kule chini (wameajiriwa) na maboresho mengine mengi ambayo yamefanyika. Tumeona ujenzi wa skimu za umwagiliaji ambao unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Isimani. Jimbo la Isimani sisi tumekuwa wa kwanza kunufanika na miradi hii ya umwagiliaji na hasa skimu za umwagiliaji. Tumepata zaidi ya shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kujenga skimu ya umwagiliaji. Kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa ambayo yanafanywa na Serikali yetu. Ninajua na maeneo mengine mengi yameendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninaomba niishauri Serikali ili kuendelea kuboresha kilimo na kiweze kuwa na tija kubwa, kwa sababu kilimo tumeona kimeajiri Watanzania wengi na kitaendelea kuajiri Watanzania wengi, wale wazalishaji na pia wote wanaoshiriki kwenye mnyororo mzima wa shughuli za kilimo. Ninaishauri Serikali kwamba iendelee kutusaidia kuweka *park house* hasa kwa wale wakulima wa maeneo ya Njombe, Iringa, Mbeya ambao wanalima mazao yenye thamani kubwa na ambayo yanatusaidia kuingiza mapato ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie wakulima wa zao la parachichi. Serikali imefanya kazi kubwa kufanya uhamasishaji, na wananchi wengi wameweza kuitikia na wanafanya kazi kubwa ya kulima na mashamba mengi yameendelea kufunguliwa, lakini changamoto kubwa ambayo tumeipata ni eneo la masoko. Tumejikuta Watanzania hawa wanalima lakini

mazao haya yanachukuliwa na watu wengine kwenda ku-*park* kwenye maeneo yao (kwenye nchi zao) na kuweka *label* zao na kuwaacha Watanzania wakipata kidogo na wao wakisafirisha nje wanapata kipato kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niishauri Serikali kwamba iendelee kutenga fedha kwenye mpango huu kujenga *park house* ambazo zitakuwa zinatumika na wakulima wadogo wadogo ambao watajiunga kwenye vikundi kwa ajili ya kwenda kutafuta masoko na kupeleka mazao hayo moja kwa moja kwenye masoko ya nje. Jambo hilo linawezekana kwa sababu tumeshaoneshwa njia, na kuna baadhi ya Watanzania wachache ambao wanafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye eneo hili la kilimo ninaiomba sana Serikali iendelee kuzisimamia idara zile za kilimo kule chini bado zinalegalega katika kuwasaidia wananchi kuweza kupata elimu ya kulima kisasa na kitaalamu zaidi ili waweze kupata mapato mazuri. Kwenye hili kweli kuna changamoto kubwa. Pia, Serikali iendelee kuwekeza kwenye utafiti wa mbegu, utafiti wa viuatilifu, na teknolojia ambayo itatuwezesha kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, katika eneo hili la kilimo Serikali ni wakati sasa wa kwenda kuangalia mazao mengine ambayo yataweza kutusaidia kuleta mapato ya kigeni. Hapa nilikuwa ninaangalia kwenye mazao ambayo ni rahisi kabisa kuyalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunafahamu *aloevera*. *Aloevera* hii kwa sasa hivi ni biashara kubwa sana duniani na inaweza kulimika kirahisi sana kwenye maeneo yetu na kwa kipande kidogo tu unaweza kutoa mazao mengi zaidi. Pia, kuna *dragon fruit*. Mazao haya mawili nilikuwa ninafanya utafiti kwenye soko la dunia kuna zaidi ya shilingi bilioni 10 ziko tu ambazo tunahitaji kuzipata kupitia mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe ushauri, haya ni mazao ambayo yanachukua eneo dogo, lakini *value* yake ni

kubwa. *Dragon fruit* kwa hapa Tanzania ukienda *Shoppers Plaza* unaweza kupata tunda moja kwa shilingi 17,000. Sasa hii unakuta ina *high value* kuliko hata parachichi. Kwa hiyo, Serikali ifanye utafiti wa mazao mengi ambayo yana *high value* ili yaweze kutuingizia fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika hili niseme kwamba kama tunajikita kwenye kilimo tuangalie *component* nyingine ya utunzaji wa mazingira. Tumeona mashamba mengi yanaendelea kufunguliwa, lakini tumeona misitu yetu inaendelea kukatwa ovyo. Sasa kama tumeamua kujikita kwenye kilimo, ni muda sasa wa kuhakikisha tunatunza mazingira yetu ili tuendelee kupata mvua za kutosha, pia tuendelee kupata maji ya kutosha. Hata kama tutafanya umwagiliaji, bado tunahitaji maji. Kwa hiyo, ninaomba katika hili, Serikali kupitia Wizara husika ya mazingira, basi iendelee kutenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu, pia kutunga sheria au kukaza pale kwenye sheria za utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, sasa nizungumze kuhusu miradi ya fedha nyingi, ambayo imetengenezwa na Serikali. Fedha nyingi zimewekezwa kwenye miradi hiyo, lakini miradi hiyo bado haijaanza kutoa matokeo. Hapa ninaomba nizungumzie ile *planning* ambayo inafanywa na wataalamu wetu. Tumeona kwamba wataalamu wanavyo-*design* miradi kumekuwa na changamoto ya kushirikiana kwa Wizara tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitoe mfano kwenye eneo ambalo mimi ninatoka. Serikali imetengeneza mradi mzuri wa umwagiliaji. Ile skimu ya umwagiliaji imechukua zaidi ya shilingi bilioni 150. Mradi ni mzuri, umeshakamilika na unafanya kazi vizuri. Hapa ninaweza kusema Wizara ya Kilimo na Wizara ya Nishati walifanya kazi vizuri kwa pamoja. Ndiyo maana uzalishaji umetoka tani 70,000 na sasa hivi tunazalisha tani 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao haya sasa hivi yanachakatwa pale kwenye eneo letu kwa sababu umeme tunao. Sasa hivi mpunga na mchele kwenye eneo lile la Pawaga unauzwa kwa kilo kwa sababu kuna uboreshwaji wa viwanda vya kuchakata mpunga na wanunuzi wanafika pale. Changamoto kubwa tuliyonayo, pamoja na uzalishaji huu mkubwa ambao

tumeupata, maeneo yale hayana barabara ya kutoa mizigo kupeleka sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unashangaa inawezekanaje tuka-*design* mradi mkubwa na wa fedha nyingi kama ule na tukawa na matarajio ya kuweza kupata siyo chini ya shilingi bilioni 100 baada ya kuuza mpunga kwenye eneo lile! Hizi data nimezipata kutoka kwa wataalamu wetu ambao wame-*design* mradi, kwamba baada ya mradi kukamilika tunapata zaidi ya shilingi bilioni 100 kutoka kwenye mradi ule, lakini *component* ya kutoa *product* kutoka kwenye eneo kupeleka sokoni haikuweza kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hili ninaomba niishauri Serikali, inawezekana kuna miradi mingine kama hii, iende ikaangaliwe, iweze kukamilishiwa hiyo *component* iliyobaki, ili miradi iweze kuwa na tija ile iliyotegemewa. Kwa mradi ule wa Pawaga, iwapo barabara ile itajengwa, basi zile shilingi bilioni 100 zitaweza kuonekana na kurudi kwenye mzunguko jambo ambalo kwa sasa haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *component* nyingine ambayo ninaomba niimalizie ni suala la rasilimali watu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umeisha.

MHE. EMMANUELA K. MTATIFIKOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninashukuru sana na Mwenyezi Mungu akubariki. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri sana Mheshimiwa Emmanuela Mtatifikolo. Nilimtaja Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, tutamaliza na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

MHE. JANETH P. PINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninachukua nafasi hii ya kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo anatusimamia Watanzania katika kuboresha miundombinu mbalimbali, tukianzia na afya, maji, barabara, elimu na mambo mengine. Kwa kweli ninachukua nafasi hii kumpongeza sana mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, ninachukua nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Mipango na Uwekezaji katika kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kusimamia masuala mbalimbali ya mipango ya kuendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele vya mipango ya uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2027/2028, na mpango wa Dira 2050, huwezi ukaacha kuzungumzia suala zima la bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa niende moja kwa moja kwenye suala la bima ya afya. Ninaipongeza sana Serikali ambayo kwa kweli wamefanya jitihada za kutekeleza suala la mpango wa bima ya afya toka awamu ya kwanza ya uandikishaji ambayo iliwahusu wananchi wale wasiokuwa na uwezo na likafanikiwa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu idadi ya wananchi waliokuwa wameandikishwa ilikuwa haizidi asilimia nane, lakini toka mpango huu ulivyoanza mwezi Februari mpaka kufikia sasa, tumepiga hatua kubwa mpaka kufikia 10% ya watu walioandikishwa na bima ya afya kwa wale wa kima cha chini pia na watu wengine. Kwa hiyo, tumepiga hatua kubwa sana katika hili suala ambalo alilisimamia mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili, imezinduliwa juzi kule Mtwara, lakini siyo Mtwara peke yake, mikoa yote, bima ya afya awamu ya pili imezinduliwa kwa uandikishaji wa wananchi wote. Katika hili halitaweza kuwa na tija kama hatutaweza

kulisimamia, wananchi wengi wakajiunga na bima ya afya, ili tuweze kupata matokeo chanya. Ninaiomba Serikali, katika suala hili la bima ya afya, tuweze kulipa kipaumbele na kulifanya kuwa ajenda muhimu katika mikoa, wilaya, kata na hata vijiji, kuzidi kutoa elimu kuhusiana na suala la bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi bado hawafahamu suala zima la bima ya afya. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali kuendelea kutoa elimu kwa Watanzania, waifahamu bima ya afya, na pia waweze kukata ama kujiunga na kutumia bima za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika umuhimu wa bima ya afya, kwa sasa hivi tulivyouzindua huu mpango wa bima ya afya, ninawapongeza sana Wizara, wameleta mpango ambao unaweza kurahisisha maisha ya Watanzania kujiunga na bima za afya; kukata bima kwa shilingi 150,000 kwa kaya ya watu sita. Kwa hiyo, ninaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutoa elimu, kiwango hiki kwa kaya ni kiasi kidogo sana, lakini Watanzania wanaweza kupata huduma za msingi zote kuanzia ngazi ya zahanati na kwa rufaa mpaka ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kuisisitiza sana Serikali kuendelea kutoa elimu kwa Watanzania kuona umuhimu wa bima hii ya afya. Huku nyuma bado kuna watu wengi na kundi kubwa ambalo limeachwa, halijaweza kujiunga na bima ya afya ipasavyo kama watumishi wa taasisi mbalimbali za binafsi pamoja na kampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la elimu, ninaomba kuendelea kuishauri Serikali kuendelea kuwaelimisha Watanzania katika suala zima la magonjwa sugu. Magonjwa sugu ni tatizo ambalo linaendelea kuutafuna mfuko kwa sababu wananchi wengi wanaumwa magonjwa haya yasiyokuwa ya kuambukiza, lakini hawana uwezo wa kujitegemea na kuweza kupata huduma za matibabu. Huduma hizi za magonjwa yasiyo ya kuambukiza yana gharama kubwa sana. Kwa hiyo, sisi kama Watanzania tuendelee kujifunza au kuendelea kupewa elimu ya kuacha zile tabia ambazo zinaleta magonjwa yale

yasiyoambukiza mfano, uvutaji wa sigara uliokithiri na unywaji wa pombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko mtaani sasa hivi watu wanakunywa sana pombe na kuondoa au kupunguza nguvu kazi ya Taifa lakini kibaya kuliko yote ni kwamba ndiyo jambo ambalo linasababisha magonjwa haya yasiyokuwa ya kuambukiza nayo ndiyo yanapelekea gharama kubwa za matibabu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna tabia za kutokufanya mazoezi. Wengi tunakuwa tuna tabia ya kubweteka, hatufanyi mazoezi. Haya yote yanasababisha sisi kuwa na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza. Vilevile, kuna suala zima la ulaji uliokithiri. Yaani Watanzania wengi tuna vyakula vingi, kwa hiyo, hatujiwekei ile *limit* ya kula chakula. Watu tunakula sana bila kufuata utaratibu na mpango. Kwa hiyo, tunakuwa wanene, kama mimi hapa ambaye ninajitahidi, sasa hivi nimepunguza sana ulaji. Kwa hiyo, ninawashauri na wenzangu, tujitahidi sana kufanya mazoezi, ku-*limit* chakula ili kuweza kuwa na afya bora. Haya yote yanasababisha kwa kiasi kikubwa magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika magonjwa haya, ndiyo yanachukua nafasi kubwa katika matumizi ya pesa kule kwenye vituo vyetu vya kutolea tiba, kwa sababu misamaha ni mingi, lakini ndiyo magonjwa ambayo yanatuondoa katika dunia hii na kupunguza nguvu kazi. Kwa hiyo, ninasisitiza sana au kushauri Serikali tuendelee kutoa elimu juu ya hili suala la kupunguza haya magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, katika maeneo yetu mbalimbali tunayotoka, tuendelee kushirikiana na Serikali, viongozi wa mikoa, wilaya, pamoja na kata, na hata kule chini kuelimisha wananchi kuhusiana na suala zima la bima ya afya. Watu wengi tumejiweka mbali kama hili suala halituhusu. Suala la bima ya afya ni suala zuri ambalo linamfanya Mtanzania kuwa na uhakika wa matibabu mara anapokuwa amepata shida ya ugonjwa wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri sana viongozi wenzangu Wabunge, tutakaporudi kwenye maeneo yetu, tuunge mkono juhudi za Serikali katika kuwaelimisha Watanzania kujiunga na bima za afya. Tushiriki kwenye mikutano ambayo wenzetu wanakwenda kuifanya maeneo mbalimbali katika kuelimisha Watanzania kwa sababu elimu hii inatolewa, lakini bado wananchi wengi hawana elimu ya bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mambo mengi. Baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Janeth Peter Pinda. Tunamalizia na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Ninaomba na mimi nitoe mchango wangu katika hii Bajeti ya Mpango wa Maendeleo 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu. Kiukweli Marais wanaoongoza katika nchi za uchumi wa kati ni tatizo kubwa. Kwa hiyo tunamwombea Mungu ampe uvumilivu, aiongoze nchi yetu na tutafika mwisho kwa wema. Tunamwombea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na wenzake, Naibu wake na watendaji wake wote. Pia, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake wote wawili. Leo ukiniuliza mimi kwamba tatizo la nchi yetu ni nini? Ni fedha, hakuna? Ni mipango mibaya? Nitakwambia tatizo ni usimamizi mbovu. Tatizo ni usimamizi mbovu wa fedha. Mifano iko wazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye jimbo langu. Leo kuna miradi ya barabara inafanyika, mfano mradi wa barabara ya Sanzate inaenda Nata – Mugumu. Sasa ni mwaka wa kumi, wametumbukiza pale mabilioni ya fedha, mradi umeharibika. Yaani ukienda kuutengeneza, unaanza moja. Hizo fedha zinatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimpa mtu leo barabara ya kujenga, kampuni moja inapewa barabara kumi, au tano au ishirini. Anachukua fedha huku, anapeleka huku; anachukua fedha huku, anapeleka huku, kumi! Leo tuna wale Mameneja wa *TANROADS*, shimo moja likitokea kwenye barabara linaongezeka mpaka yanakuwa mashimo 300, yupo; Waziri wa idara hiyo, yupo; Mawaziri wengine, wapo. Tatizo ni usimamizi katika nchi yetu, niwaambie ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa barabara ya Sanzate – Nata iko pale. Juzi wametoa shilingi bilioni mbili, yule mkandarasi hayupo, hajaenda na wala hakuna wa kumfuata. Ukienda kwenye hizi barabara, kuna barabara ya Bukama – Mekomariro imeahidiwa kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe na *TANROADS*, bado. Kuna hiyo barabara ya Sanzate imekuwa wimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa kwenye huu mpango tuendelee kuitengeneza hii barabara. Ushauri wangu ni nini? Maana yake ni kwamba kama tuna mpango wa kuanzisha mradi, basi huo mradi ufike mwisho halafu twende kuinadi miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukawa na miradi mingi, mingi, mingi katika hii nchi lakini haifiki, na tunaangalia tu. Mradi ulikuwa wa shilingi milioni 300, badala yake unakuwa wa shilingi milioni 700, itakuwa kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba barabara ya lami ambayo iko kwenye Ilani ya CCM ya kutoka Bariri – Mgeta, tunaomba iingie kwenye Mpango. Tuna mradi wa maji wa Butiama – Nyamuswa, umekwama uko hapa. Waziri wa Maji juzi alikuwepo jimboni kwangu, amesema atafanya kila namna fedha ziende mradi uishe. Ninamwomba asisitize zile fedha alizoahidi ziende kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa vijiji 33, jimbo zima la Bunda halina maji. Ipo Kata moja inaitwa Kitale na Kata ya Biringo hakuna hata kisima cha maji. Ninaomba mipango

iliyopangwa kwenye vijiji 33 vya mradi wa Ziwa Victoria iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama. Mipango yote tunayopanga hapa ni kwa ajili ya wananchi. Ni lazima wananchi wetu wapate mpango, wapate na usalama wa kuishi. Katika Jimbo la Bunda kuna suala la tembo. Leo siyo kwamba wanakula mashamba tu, wanaishi kwenye kaya. Watu hawaendi kuchunga, hawaendi kutafuta chakula, wako pale pale wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea, tumeongea, Waziri wa Maliasili na Utalii alikuwepo pale jimboni, tumemwambia. Tunaomba tena, kama kuna *operation* ya kwenda kufukuza tembo, waende kwenye Jimbo la Bunda kwenye Kata ya Hunyari wanaishi kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, huko tunakoenda sasa tuwe na mpango maalumu. Mfano, kuna huu mradi umekuja wa benki wa kukopesha ng'ombe waupeleke kwenye Jimbo la Bunda ambako sasa watu hawalimi, waende wakawape ng'ombe. Juzi wamekuja pale tumewapa makadirio ya ng'ombe 2,000 kwa vijiji 100, ina maana kila kijiji ng'ombe ishirini ishirini au kumi kumi ili waweze kuishi sasa, hata kama tembo watakuja, lakini watu wana maziwa kwa sababu wale ng'ombe wanafungiwa ndani; vinginevyo hali ya hatari kule ni mbaya sana. Wananchi wameshakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, tuna Sekondari ya Kurusanga, tumeiomba, watoto wanateseka. Tuna Sekondari ya Sanzate wamejenga jengo moja halijamalizika. Kuna Sekondari ya Nyamuswa, tunaomba tujengewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kujua, mikoa ya Tanzania iko 26. Hivi tuna barabara ngapi za lami zinazounganisha mikoa? Kama ziko katika hiyo mikoa 26, ni ngapi zimeharibika? Kwa maana ni lazima tutoke hapa tumetengeneza bajeti. Tuna mikoa 26, barabara zinazounganisha mikoa ni ngapi? Ngapi zina hali mbaya zaidi? Tuseme basi robo ziko vizuri. Tutengeneze bajeti ya kilometa zilizobaki. Tuje kwenye barabara za changarawe

zilizounganisha mikoa na wilaya, tujue ngapi zimeharibika? Bunge lijalo la bajeti waje watuambie shilingi bilioni au shilingi trilioni 12 au 13 au 16 zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na wilaya. Sasa vinginevyo tutakuwa tunaimba tu humu ndani. Tutaimba mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kukwambia, sisi kama hatushughulikii matatizo ya wananchi, hata huko tunakokwenda kuna Wabunge tutakuwa tunaogopa kwenda kuomba kura. Unaomba nini? Unaomba nini watu wako wanateseka kila siku? Watoto wengine wanakaa chini hawana madawati, maeneo mengi tu. Mpaka wa sekondari nao wanakaa chini, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba hii mipango ya kushukulika na wananchi, madawati ya wanafunzi wa shule za sekondari na msingi, barabara na maji, tuitengenezee muundo mzuri ili wananchi wetu waweze kuwa na imani. Vinginevyo hapa tutajidanganya tu, tutaimba humu ndani, wazuri, wazuri; huko nje itagoma. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, huyu alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

Katibu.

NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa orodha ya shughuli ya siku ya leo. Hivyo, ninaahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu tarehe 2 Novemba, saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.17 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu Tarehe 2 Novemba, 2026 Saa Tatu Asubuhi)